

YEHOVA-YIRE ²



Hebu na tuendeleo kusimama, kwa dakika moja, tunapoinamisha vichwa vyetu.

² Baba wa Mbinguni, tunashukuru, usiku wa leo, kwa nafasi tuliyo nayo, kuja tena katika nyumba ya ibada, ambamo tunajihudhuria na shida zetu Kwako, kwamba uliahidi kukutana nasi hapa chini ya Damu iliyomwagika. Mahali pekee palipoandaliwa ambapo Mungu alipata kuwa napo ambapo mwenye dhambi, ama mtu yeyote angeweza kukutana na Mungu, palikuwa ni chini ya Damu iliyomwagika. Kwa hiyo tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, tukijua ya kwamba Wewe uliahidi iwa—iwapo tungeomba jambo lolote katika Jina hilo, hatuna budi kupewa. Tunakuamini Wewe, Baba. Tusaidie kutokuamini kwetu. Tunaomba ya kwamba kukusanyika kwetu pamoja, usiku wa leo, kutakuwa ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwamba Mungu apate kuadhimishwa, na Jina Lake litambulikane miongoni mwa watu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

Mwaweza kuketi.

³ Ninahesabu haya kuwa ni majaliwa kuwa hapa tena usiku wa leo, na kuliona kundi hili zuri la watu waliokusanyika hapa nje. Ninaamini, walisema yalikuwa ni maonyesho ya mifugo. Nimefanya mikutano, takribani, sehemu za kila aina kote ulimwenguni. Ninakumbuka kule California, nimekuwa na mikutano miwili ama mitatu kwenye Ikulu ya Ng'ombe, wanavyopaita. Na kutoka maeneo yenye ukubwa mbalimbali, chumba chenye nafasi ndogo inayotosha watu watano ama sita, hadi kufikia, vema, kusanyiko kubwa sana tulilopata kuwa nalo kwa wakati mmoja, ilikuwa ni huko Bombay, mia tano elfu kwenye kusanyiko moja.

⁴ Lakini, huko Bombay, jambo muhimu, Bwana wetu aliwaokoa watu wengi. Iwapo tungeweza tu kuyafanya makanisa yawe na ushirikiano, wangeliwachukua hao Wahindu na kadhalika. Na hao walikuwa kwa kweli ni, tunaowaita, “wasioamini.” Chochote kisichomwamini Bwana Yesu Kristo, tunamwita huyo “asiyeamini.” Na kulikuwa na maelfu dhahiri waliomkubali Kristo, bali ungeweza...kamwe tusingeweza kuwafikia.

⁵ Halafu huko Durban, Afrika Kusini, tulihasabu kule, hao watu, elfu thelathini kwenye wito mmoja wa madhabahuni, alasiri moja. Ambapo, kesho yake, meya, Sidney Smith, wa Durban, akiwa na kama hayo malori makubwa saba ama manane ya Kiingereza yamejaa mpaka juu mikongojo iliyochakaa na kadhalika ambayo watu hao walikuwa

wametembelea, kwa mamia ya maili. Ama, waliwaleta kwa majuma kadhaa, wakija kupitia misituni, kwenye machela. Yalikuwa yote yamejaa hayo.

⁶ Meya alinipigia simu, kasema, “Nenda kwenye dirisha lako linaloelekea kwenye Bahari ya Hindi, huko nje hotelini,” kasema, “nawe utaona jambo ambalo hujawahi kuliona.”

⁷ Na hapa yalikuwapo hayo malori makubwa yamejaa tele, ambayo tungeita, mikongojo na machela, na kadhalika, kuwabebea wependwa wao kutoka misituni. Na watu waliokuwa wamebebwa nayo, siku iliyotangulia, walikuwa wakitembea nyuma ya lori, wakiimba *Amini Tu* katika lugha yao ya kienyeji. Ilikuwa kweli ni onyesho la kuvutia sana kuona jambo hilo.

⁸ Na kati yao kulikuwa na madaktari. Wengi wao walichunguza visa hivyo, kuhakikisha ya kwamba vilikuwa ni vya kweli. Hatutaki kuandika chochote, ama kuchapisha chochote, isipokuwa kiwe kinaweza kuthibitishwa, kwamba ni kweli. Hakina budi kuthibitishwa!

⁹ Hivi punde nimepata barua kutoka kwa ninii . . . muda mfupi uliopita. Nimekumbuka tu sasa hivi. Ni daktari maalumu, anayejulikana sana Indiana. Yeye ni Mkatoliki, kwa imani. Na mwanawe ni kasisi kwenye Nyumba ya Utawa ya Mt. Meinard huko Jasper, Indiana. Huyu alikuwa ni Dk. C. Ackerman. Nami ilitokea kwamba nilikutana naye kwenye ziara ya kuwinda, wakati mmoja. Naye alikuwa amewinda kwa muda wa miaka kumi na mmoja, apate kulungu. Alishindwa kumpata mmoja. Na usiku huo, tuliketi mpaka karibu saa nane, tukizungumza habari za Bwana.

¹⁰ Nilisikia daktari huyu alikuwa huko juu kambini. Kwa hiyo wakati nilipofika huko, nilikuwa nikitarajia kukutana na mtu mwenye majivuno na asiyejali. Lakini nilikutana na mtu mzuri sana, mchangamfu. Alikuwa, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam, bwana, ni mimi.”

Naye akanipa mkono. Akasema, “Mimi ni Dk. Ackerman.”

Nikasema, “Vema, hakika nina furaha kukufahamu.”

¹¹ Tukaanza kuzungumza habari za Mungu, na kuhusu ambavyo kama Yeye alikuwa ni Mungu, hana budi kubaki kuwa Mungu, vinginevyo, hajawahi kuwa Mungu. Unaona? Mungu wa historia hafai kitu leo, kama Yeye si yeye yule kwa watu leo kama alivyokuwa wakati huo.

¹² Kwa hiyo, yapata kama saa tisa, sisi, loo, ki—kiongozi alitumsha. Na nilikuwa . . . Nilikuwa nikiongoza, pia, kwa hiyo tulikuwa tunaanza safari, kuwapeleka watu wetu sehemu mbalimbali ambako tungewaongoza njia. Tulipokuwa tukishuka kwenda zetu, Dk. Ackerman alikabidhiwa kwangu.

13 Basi tulipokuwa tukishuka barabarani, alisimama, kidogo kabla ya mapambazuko. Akaweka mkono wake juu ya bega langu, kasema, “Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam, bwana, daktari.”

14 Akasema, “Mimi nimeshawishika kabisa juu ya Yesu Kristo.” Akasema, “Nina mvulana, unajua, yeye ni kasisi hapa kwenye nyumba ya watawa.”

Na nikasema, “Ndiyo, bwana.”

15 Akasema, “Mimi ni Mkatoliki, kwa imani. Nadhani ni kanisa hilo.” Binafsi akasema, “Vema ninaamini kama—kama Yeye alipata kuwa Mungu, Yeye ni Mungu wa watu wote.”

16 Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa. Yeye aliumba watu wote. Na kwa Damu moja aliyafanya mataifa yote.”

17 Naye akasema, “Naam, bwana, ninaamini hilo.” Kasema, “Nimesoma vitabu vyako.” Akasema, “Ninakwambia jambo hili kisiri. Ninaamini, kama utamwomba Mungu, anipe kulungu leo, nitampata.” Kasema, “Nimewawinda kwa muda wa miaka kumi na mmoja; nimenaswa kwenye dhoruba za theluji.”

18 Nikasema, “Nitamwomba Bwana akupe mmoja, daktari. Hivyo tu ndivyo ninavyoweza kufanya.” Ndipo nilipomwomba, nikamwombea. Nikasema, “Daktari, mnamo saa tatu kamili, asubuhi ya leo, Bwana anakupa kulungu dume ki—kipimo nukta tano.”

Naye akasema, “Ninaamini jambo hilo.”

Hivyo tu ndivyo anavyopaswa kufanya. “Kama ukiamini.”

19 Kwa hiyo, mimi na rafiki yangu mmoja, tulipanda kilima, na kulinda zamu. Saa tatu bunduki ikalia. Alimpata kulungu dume wa nukta tano. Tulienda tukamsaidia kumwingiza ndani.

20 Yeye huwaleta wagonjwa wake waombewe. Sasa hivi nimepata habari ya dharura, ya kwamba ana mgonjwa wa kansa, mwanamke anayekufa kwa kansa, angetaka kumleta huku kwa ndege. Lakini ninaenda nyumbani, baada ya kesho, baadaye, kesho kutwa. Kwa hiyo nikamwambia, angoje tu mpaka tutakapofika kule, tungemwombea mwanamke huyo tutakapofika kule.

21 Kwa hiyo, unaona, wengi, laiti mtu angaliweza kuelezewa kisa hicho vizuri! Uponyaji wa Kiungu umezungumziwa sana, na ushupavu mwingi wa dini ukaingizwa ndani yake, kama vile ilivyo kwa vitu vingine vyote. Di—dini ya namna yoyote ama chochote kile, unapata washupavu wake.

22 Hata kwa Waislamu, unapata wako, na Wahindu. Unakuta mtu fulani kule, shabiki mnafiki akifanyia watalii vitimbi, akilala juu ya misumari na kadhalika, gilasi. Bali kule ndani barani, yupo mtu ambaye kweli anaamini katika hayo. Anafanya hayo kwa ajili ya sadaka.

²³ Na—na tunaona jambo hilo katika kila kitu. Tunakuta ushupavu. Hata mshupavu mlaji hula kupita kiasi. Ama, ama, chochote kile!

²⁴ Lakini kama kisa hicho kikielezewa katika Maandiko, basi hakuna chochote kinachoweza... Ninakuta madaktari wengi zaidi wanaoamini kuliko ninavyowakuta wahudumu. Ninawakuta. Kweli ninawakuta. Wengi zaidi wanaamini.

²⁵ Nimehojiwa huko kwa Mayo. Kama nyote mnajua jambo hilo, limeenezwa kote na magazeti, na kila kitu. Na kliniki nzuri za madaktari kila mahali. Hakuna kitu. Wao wanaamini. Ni—nimekuwa na madaktari ambao wamekuja wakaniambia, kama vile ilivyokuwa kwenye mahojiano kule, wakisema, “Sisi hatudai kuwa waponyaji. Tunadai kuyasaidia maumbile. Kuna mponyaji mmoja tu; huyo ni Mungu.”

²⁶ Ni wangapi waliosoma *Reader's Digest*, juu ya maskini mtoto Donny Morton, ambaye wamentilia sahihi, “aliponywa”? Na, “Mwujiza wa Donny Morton,” *Reader's Digest*. Kwa hiyo, hao, hao walinihoji juu ya jambo hilo. Maskini mvulana huyo mdogo alikuwa amekatiwa tamaa na Mayo, Hopkins, na hao wote. Naye Bwana Yesu akamponya, akamfanya mzima.

²⁷ Na Florence Nightingale, mjukuu wa kike wa hayati Florence Nightingale, London, Uingereza. Alisafirishwa kwa ndege kutoka Durban, Afrika Kusini.

²⁸ Pia jambo hilo limewakilishwa vibaya. Kama vile tu ninii... kama vile mara nyingi katika...

²⁹ Nao Ukristo unawakilishwa vibaya kwa watu. Ukristo umewakilishwa kwa watu kama azimio la kanuni ya imani. Ukristo ni Kiumbe kilicho hai, Yesu Kristo, Mungu aliyefufuka, aliye hai na yupo miongoni mwetu sasa. Ukristo ni Mtu, sio kanuni ya imani. “Kumjua Yeye ni Uzima.” Si hata kujua Neno Lake; huo si Uzima. “Kumjua Yeye,” Naye ni Neno.

³⁰ Mtu fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, alisema... Nilikuwa tu nikizungumzia kuhusu ninii... juu ya mambo yale tuliowazia kuhusu Maandiko fulani katika Biblia. Mtu huyu alikuwa ni msomi hasa. Akasema, “Vema, ni kwamba tu wewe huijui Biblia yako.”

³¹ Nikasema, “Ninamjua Mwandishi wake vizuri sana.” Kwa hiyo, hilo ndilo jambo muhimu, kama ninamjua. Yeye atashughulikia mengine yote. “Kumjua ni Uzima.”

³² Na, sasa, kesho asubuhi, humu jengoni, hapo, mtu wangu wa uhusiano wa jamii, Dk. Lee Vayle, yupo hapa. Kukiwa na maswali moyoni mwako, njoo, atayajibu, atafanya chochote awezacho, kuwasaidia. Dk. Vayle yupo hapa. Ninaamini yuko mahali fulani nyuma ya jengo sasa. Msomi hodari sana, na ni mtu aliyefunzwa vizuri sana kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, kama mtu yeyote ana swali, ama chochote kile, na badala ya

kujaribu tu kuliuliza sasa, katika mkutano wa watu wote kama huu, mbona, mwone Dk. Vayle. Atafurahia kuzungumzia juu ya jambo lolote ambalo—ambalo ungetaka kuzungumza naye. Na pia ana ibada hapa, asubuhi. Nasi tungefurahia ku—kukutana na watu hapa.

³³ Na, kisha, Jumapili asubuhi itakuwa ni shule ya Jumapili, kote mjini. Hatuninii—hatujaribu kuchukua Jumapili, Jumapili asubuhi ama Jumapili alasiri, kwenye ukumbi huu wa mikutano hapa, kwa sababu si—si sawa.

³⁴ Mnaona, makanisa, ninii—wajibu wenu ni huko kanisani mwe—mwenu. Na wakati kanisa linapokuwa na ibada, hu—huko ndiko kunapaswa kuwa mahali penu. Nasi hatutaki mtu yeyote aje huk, wakati ukiwa na mahali pako pa kuhudhuria. Kama kanisa lako lina ufufuo, na itokee kwamba sisi tufike kwenye mji huo mahali ambapo mnaofanyia huo ufufuo, hatumaanishi kufanya hivyo, hata kidogo. Tuko hapa katika ushirika wa Kikristo, kuvumiliana, kwa nia njema kwa watu wote, makanisa yote. Hatuninii. . .

³⁵ Mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, hata kidogo. Mimi si mfuasi wa shirika lolote. Mi—mimi ni Mkristo tu. Nami, ushawishi nilio nao, ninajaribu tu kuutumia ku—kumwadhimisha Kristo, na kuwaleta wenye dhambi wakatubu. Na hayo tu ndiyo ninayojua kufanya. Nikitumaini, kwenye ile Siku, na nikitumaini ya kwamba Yeye atasema, “Ulifanya vema.” Na hayo ndiyo maneno ninayotaka kusema. . . kumsikia akiyasema.

³⁶ Mara nyingi nimeshangaa. Ningalipenda kumsikia wakati aliposimama na kuinyosha mikono Yake siku ile, na kusema, “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo.” Sasa, hilo lilikuwa ni wakati uliopita. Lakini, “Vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu,” itakuwa ni siku za usoni. Na, mimi, ninaishi nipate kusikia hilo likisemwa.

³⁷ Na sasa, basi, Jumapili alasiri, tutawaombea wagonjwa. Mara nyingi watu wanakuita huko kwamba ni ibada za uponyaji. Sasa, si ibada ya uponyaji. Ni kuwaombea wagonjwa. Mnaona? Tunawaombea wagonjwa. Na, kwa kawaida, hapo ndipo mambo yanapotukia, ni wakati tunapowaombea wagonjwa.

³⁸ Ninamtaka kila mhudumu, kote nchini, popote pale, ambaye anaamini, aje, ahakikishe amekuja Jumapili alasiri, asimame pamoja nasi tunapowaombea wagonjwa. Bila kujali madhehebu yako ni yapi, ama yoyote yale, hatujali juu ya jambo hilo. Hakika, unawahurumia watu wako, na kwa ajili ya watu ambao ni watu wa Mungu, na watu wanaotaka kuponywa.

³⁹ Kumbuka, unapokuwa mgonjwa, jukumu lako la kwanza ni kumwona daktari wako na kuona anayosema. Halafu basi kama akitambua ugonjwa wa kitu fulani ambacho—ambacho hawezi; sayansi, sayansi haijaweza kumfunulia msaada wowote kwa ajili

yako, basi una haki ya kumjia Mungu. Yeye ndiye Tabibu mkuu. Halafu basi. . .

⁴⁰ Pia uombe, na uombewe. Wanafanya jambo hilo, wanapaswa kulifanya, katika kila kanisa la Kikristo. Labda, wanafanya hivyo hapa. Sijui. Bali mahali pengi, Wakristo huwaombea wagonjwa wao. Wapresbiteri na wengi wao wana mikutano mikubwa ya uponyaji kote kaskazini, na sehemu mbalimbali nchini, wakiwaombea wagonjwa, na wanapata mafanikio makubwa; Presbiteri, Lutheri, Methodisti, mengi yao.

⁴¹ Ufufuo wao mkuu ulianza kwa miamsho ya uponyaji. Nao wakaiacha, hakika. Kundi jipya linaingia, wao, kundi la watu linakutanika na kuligawanya jinsi linavyotaka kuligawanya, halafu wanaiacha, mnaona, wamarudi moja kwa moja kwenye hiyo kanuni ya imani, kama vile Mafarisayo na Masadukayo wa wakati wa Bwana Yesu.

⁴² Lakini sasa, kila mhudumu anakaribishwa, Jumapili alasiri, aje awe pamoja nami, na—na kunisaidia tukiwaombea wagonjwa. Waleteni wagonjwa wenu na wanaoteseka.

⁴³ Sasa, tunajaribu sasa kuwafanya watu. . . wawatafute wenye dhambi wasiomjua Bwana wetu, wasiotambua ya kwamba Yeye hajafa. Yeye yu hai. Yeye, Yeye hajafa. Yu hai, milele. Naye alisema, “Kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtaishi pia.” Ni ahadi ya jinsi gani, na ni faraja ya jinsi gani, tunapooni wakati ukikaribia!

⁴⁴ Wakristo wote halisi wanaamini ya kwamba Kuja kwa Kristo Mara ya Pili kumekaribia. Kwamba ni muda gani, hatujui. Je! mliona Alaska ikiwa na matetemeko mengine kadhaa ya ardhi leo? Moja la hayo, lilikuwa lenye nguvu sana kama lile la kwanza lilivyokuwa, ila tu halikuizamisha. Mwajua, Yesu alisema mambo ya namna hiyo yangetukia kabla tu ya Kuja Kwake.

⁴⁵ Na, kumbukeni, mambo haya mnayoona yakitukia hapa, Neno lilibashiri yangukuwa hapa, kama tu vile alivyobashiri lile tetemeko la ardhi. Kwa hiyo, pamoja, kwa nini tusiweke tu mioyo yetu pamoja, na tuifunge katika Neno la Mungu, na kuamini kwa mioyo yetu yote? Vema.

⁴⁶ Sasa, jana usiku, tulikuwa. . . Nilichukua somo la Ibrahimu, wakati alipoliitia Jina la Bwana aliyemtokea huko juu kwenye sadaka ya mwanawe, alikuwa akienda. Jina hilo lilikuwa ni *Yehova-Yire*, ambalo ni, “Bwana atajipatia Mwenyewe sadaka.”

⁴⁷ Sasa, usiku wa leo, nina Maandiko machache na mihtasari, ama miwili, iliyoandikwa hapa chini, ambayo ningetaka kuacha—kuwaachia. Sasa, kabla tu hatujafanya jambo hilo, hebu na tuombe kwa dakika moja, tena.

⁴⁸ Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utachukua Neno Lako. . . “Neno Lako ni Kweli.” Nayo Biblia ilisema, Yesu

akizungumza, alisema, “Neno ni Mbegu ambayo Mpanzi alipanda.” Sasa tunatambua ya kwamba kama mbegu ni mbegu nzuri, inachipuka. Na kama mbegu hiyo imetekeleza, iko—iko kwenye mpango wa mapenzi ya Mungu, basi inaacha mbegu iliyochipuka. Na wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alikuwa ni ule Mzabibu. Na mbegu aliyoipanda ilikuwa ni Neno Lake, nasi tunajua ya kwamba imehuishwa na Uhai Wake Mwenyewe.

⁴⁹ Nasi tunajua ya kwamba mbegu, inapoanguka katika ardhi nzuri; si juu ya miamba, bila mizizi; wala katika miiba na michongoma, ambayo karibuni ingeisonga; bali katika imani nzuri, izaayo kwa wingi, yenye rotuba. Kila mbegu itazaa kwa jinsi yake.

⁵⁰ Nasi tunajua ya kwamba kila mbegu, ama ahadi ya Mungu, itazaa kwa jinsi yake, kile ilichoahidi, kama ikiingia kwenye ninii . . . ardhi nzuri, ardhi iliyolimwa, iliyo tayari; ma—mawe yote yametupiliwa mbali, na mashina, na uchungu, na uchoyo, na kutojali, na wivu, vyote vimepekuliwa vikatupwa nje; hilo shina la uchungu linalozuka, ambalo mara nyingi huharibu jambo ambalo Mungu anajaribu kufanya. Tunaomba, Mungu, ya kwamba hayo hayatakuwa miongoni mwetu, bali kwamba Neno zuri litapata ardhi nzuri ndani ya hawa.

⁵¹ Tunapomfuatilia huyu mzee wetu maarufu, Ibrahimu, katika somo hili usiku wa leo, jalia tuone nafasi yetu, tukijua ya kwamba sisi ni wana wa Ibrahimu, kwa imani katika Kristo. Na, halafu, ujipatie utukufu kwa Jina Lako Mwenyewe na heshima, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁵² Kwa namna fulani tutarejea nyuma kidogo usiku huu, kwa lile somo la yale tuliyokuwa tukizungumzia jana jioni. Hiyo ilikuwa, kwamba, tulimwona Ibrahimu akianza, katika Mwanzo mlango wa 12. Kwa kweli, jina lake lilitamkwa katika mlango wa 11, wakati baba yake aliposhuka akaja kutoka Babeli nao wakaishi katika—katika Uru na hii . . . nchi ya Wakaldayo.

⁵³ Na ndipo tunaona ya kwamba, pia, ya kwamba Mungu alimwita Ibrahimu, mtu wa kawaida tu aliyeitwa Abram. Hakuwa Ibrahimu bado. Na, na Sara, “Sarai,” Sara hakuwa Sara bado. Kwa hiyo tunaona, *Sarai* na *Sara* yalikuwa mawili tofa . . . yalikuwa majina mawili tofauti. Na *Abramu* na *Ibrahimu* yalikuwa ni majina mawili tofauti.

⁵⁴ Sasa tunaona ya kwamba, katika jambo hili, tulimleta jana usiku, mpaka kwenye kuthibitishwa, ambapo Mungu alimthibitishia lile agano, jinsi ambavyo angemthibitishia Ibrahimu ya kwamba atatimiza ahadi Yake. Hilo linapatikana katika mlango huu wa 15 wa Mwanzo. Jinsi ambavyo . . . Naye Ibrahimu aliitwa wakati wa jioni, kumwangusha, kumchinja ndama ama mtamba, na mbuzi jike, na kondoo dume. Nasi tuliingilia jambo hilo jana usiku, jinsi ambavyo wale wa kike wawili na wa kiume. Na halafu wale hua wawili, ama njiwa

na hua, ambao ni familia moja; na tukapata uwakilisho wa hao, ya kwamba hao daima waliwakilisha uponyaji. Ambao, kamwe haukubadilika. Uponyaji daima umekuwa ni kwa imani. Lakini ule upatanisho, hakika, uligawanywa toka kwenye uhai wa mnyama ukaingizwa katika uhai wa mwanadamu.

⁵⁵ Sasa, katika Agano la Kale, wakati mwabuduo alipokuja na damu. Mungu hukutana tu na watu chini ya Damu iliyomwagika, mahali pekee alipowahi ama atakapowahi kukutana nao. Kamwe hatakutana nawe pamoja na kanuni yako ya imani. Hatakutana na wewe kamwe na elimu yako. Atakutana nawe chini ya Damu; hapo ndipo mahali pekee. Israeli wote waliabudu chini ya damu.

⁵⁶ Na tunaona pale basi, pia, ya kwamba tulikuta (nini?) huko nyuma katika historia ya vile, jinsi ambavyo agano lilivyofanywa na watu, na tunaona katika mfano wa watu wa Mashariki na njia mbalimbali wafanyavyo agano. Na jinsi tunavyofanya siku hizi, kwa kupeana mikono, na kadhalika, na kusema, “Litie muhuri!” Nao Wajapani wanarushiana chumvi, kwa ajili ya agano.

⁵⁷ Na—na kusafiri kote ulimwenguni, na unakuta ulimwengu karibu wote ungali katika hali ile ile uliyokuwa nayo huko nyuma katika siku hizo, hasa sana katika nchi za Mashariki ya Mbali na katika Mashariki. Biblia yako inakuwa kitabu kipya kama ukiwahi kwenda huko Mashariki, kamwe hutaninii... huko Yerusalemu, Palestina, huko nyuma. Mtaninii... Biblia, imeandikwa katika ninii... Sisi ni Waingereza huku, na watu wa Magharibi, tukijaribu kuelewa kitabu cha Kiingereza, kwa hiyo ni jambo gumu sana. Kama ukirudi huko nyuma, utaona ndoa na kila kitu, na vile hasa walivyoifanya katika zama za Kristo. Mambo mengi kule hayajabadilika hata kidogo, katika utamaduni wao na njia zao.

⁵⁸ Na sasa sisi, katika jambo hili, tunaona ya kwamba wakati walipofanya agano hili katika siku hizo, wali—walilichora kwenye kipande cha ngozi ya kondoo, ama—ama ngozi. Na kisha wakamchinja mnyama, na wakasimama katikati ya vipande hivyo. Nao wakampasua, hili ni agano lao, ama katika vipande viwili, maneno yao; wakampasua vipande viwili, namna *hiyo*. [Ndugu Branham anapasua kipande cha karatasi vipande viwili—Mh.] Na wakati vilipoumanishwa, *hivi* vilipaswa kumana vivyo hivyo kabisa. Ilibidi vikutanishwe, kipande kwa kipande, hivi kwamba havingeweza kunakiliwa. Kwa hiyo basi tunaona, ya kwamba, katika somo letu jana usiku, tuliona hivyo ndivyo Mungu alivyofanya kumthibitishia Ibrahimu agano Lake.

⁵⁹ Sasa, Ibrahimu, ahadi ilifanywa kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Si kwa Ibrahimu peke yake, bali Uzao wake. Sasa, sasa, ule uzao, uzao wa kawaida wa Ibrahimu, ulikuwa ni Isaka; bali Uzao wa kiroho wa imani ya Ibrahimu,

ulikuwa ni Kristo. Si kupitia kwa Isaka, ambapo ulimwengu wote ulibarikiwa; bali kupitia kwa Kristo, Uzao wa Kifalme, ulimwengu wote ulibarikiwa, kwa maana alikufa kwa ajili ya watu wote, mataifa yote na watu wote.

⁶⁰ Sasa tunaona katika jambo hili, pia, katika agano hili, ya kwamba Yeye alionyesha pale yale angefanya, jinsi ambavyo Mungu angempasua Kristo Yesu vipande viwili. Na mwili huo ulifufuliwa na unaketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu na Ukuu huko Juu, Naye Roho wa Kristo akashushwa juu ya nchi.

⁶¹ Sasa kama tungalikuwa na wakati, ungeweza kuthibitisha jambo hilo. Chochote, sehemu moja ya Maandiko ikisema, inaenda kote katika Biblia. Ispoenda, basi kuna—kuna kasoro fulani. La Kale lilikuwa tu ni kivuli cha lile Jipya, kutangulia kulionyesha. Basi, ukipata kivuli, unaweza kujua vizuri sana kile lile Jipya lilivyo. Kwa hiyo hapo ndipo alipokuwa, alipo, na atakapokuwa.

⁶² Sasa Roho huyu wa Kristo alirudi juu ya Kanisa, akatimiza Yohana 15 kikamilifu tena, ambapo Yeye alisema, “Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Na halafu tena, Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya,” kazi zile zile, jambo lile lile. Na kuendelea kote katika Maandiko! “Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu likae ndani yenu; ombeni mtakalo, mtapewa.” Mambo mengi ambayo Kristo . . .

⁶³ “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hilo *ulimwengu*,” hapo neno la Kiyunani ni *kosmos*, ambalo maana yake ni *utaratibu wa ulimwengu*, “hautaniona tena. Bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” *Mimi* kikiwa ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilfu wa dahari,” ikimfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye—Yeye—Yeye anadumu. Alifufuka katika wafu. “Ulimwengu, asiyeamini, hataniona.” Hawatatambua jambo Hilo. Lakini mwaminio atamtambua Yeye, kwa sababu ni Yesu yule yule aliyekuwa daima. Hajabadilika. “Yeye yule jana, leo, na hata milele!”

⁶⁴ Na sasa, na Neno hilo, watu wengi wanajaribu kulifanya Hilo kana kwamba halijavuviwa. Sasa, ninataka kusema jambo fulani hapa sasa, limekuja tu niani mwangu.

⁶⁵ Wala siamini ya kwamba mimbara imefanywa kwa ajli ya mahali pa mizaha. Hapa si mahali pa kufanyia mizaha. Huu ni uaminifu. Na tunapoona Siku ya Bwana ikijitokeza, tunapaswa kuwa waaminifu zaidi.

⁶⁶ Lakini kuna ha—hadithi niliyopata kusimuliwa, muda fulani uliopita, juu ya ja—jamaa mdogo ambaye . . . Hii ilikuwa ni huko Boston, naye akaondoka. Alikuwa na mama mzuri, kwanza, kuianza hiyo hadithi, naye mama huyo kwa kweli alijua huyo mvulana wake alikuwa na wito maishani mwake, kumtumikia

Bwana. Na hiyo ingeninii—hiyo ingemsaidia mama yeyote, inapaswa kumsaidia, mama yeyote halisi, kujua ya kwamba mtoto wake wa kiume... ya kwamba Mungu amewatunukia mtoto ambaye ataihubiri Injili. Hiyo inapaswa kuwa ni rasilimali kwa maisha ya mama yeyote. Na kwa hiyo maskini mama huyo, akijaribu kufanya yote angaliweza, alimpeleka shuleni, halafu seminari, akapate BA ya—yake.

⁶⁷ Na kwa hiyo wakati alipokuwa ameondoka, mama huyo aliugua sana. Na basi huyo mama, kama vile ambavyo Mkristo yeyote angefanya, walimwita daktari. Naye daktari... Alikuwa na nimonia maradufu. Naye daktari alijaribu yote aliyoweza kumfanyia, ku—kuidhibiti hiyo nimonia, wala haikufaa chochote. Alikuwa amempa dawa za—za salfa, penisilini, na kadhalika, ili ku—kuua vijidudu hivyo, nayo haikufanikiwa. Mama huyo alizidi kuwa na hali mbaya zaidi, wakati wote. Kwa hiyo wakamtumia taarifa mwanawe, ambaye alikuwa mbali huko Asbury, Kentucky, kwenye Chuo cha Wilmore, kuja kumtembe... kumwona kwa sababu alikuwa anaenda kuaga dunia. Na ndipo kesho yake asubuhi, wakati mvulana huyo alipokuwa akijitayarisha kuondoka, walipata barua ya simu, “Mama yako hajambo sana. Ngojia uitwe tena.”

⁶⁸ Yapata mwaka mmoja baadaye, mwanamke huyo alikuwa na majaliwa ya kumwona mwanawe. Alirudi nyumbani kwa likizo na ulikuwa ni muda wake wa kutoka shuleni mwake. Ndipo akasema, “Mama, nilisikia ya kwamba ulipona,” baada ya wao kuwa na wakati mfupi wa ushirika, kama vile ambavyo mwana na mamaye wangepanya. Kasema, “Ka—kamwe sikuelewa kabisa ni dawa gani hasa huyo daktari alibadilisha, kufanya hali ya—yako kubadilika upesi hivyo.”

⁶⁹ Naye akasema, “Mwanangu, si—sivyo ilivyokuwa.” Akasema, “Je! unajua mahali ile misheni ndogo ilipo hapa chini mtaani, hao watu kule chini ambao...”

Kasema, “Ndiyo, ninaikumbuka hiyo.”

⁷⁰ Kasema, “Kuna mama mmoja aliyesema ya kwamba alijisikia akiongozwa kuja hapa na kuniomba kama mchungaji angeweza kuja na kuniombea. Na kwa hiyo nikamwambia ilikuwa ni sawa.” Kwa hiyo akasema, “Mchungaji alikuja na kusoma jambo hilo kutoka kwenye Biblia, ‘Mtu yeyote miongoni mweni, akiwa mgonjwa, awaite wazee, na kuwapaka mafuta; wawaombee. Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa.’” Kisha akasema, “Unajua, alisoma hayo kutoka katika Maandiko, kisha akaniombea na kunipaka mafuta. Na—na kesho yake asubuhi, nilikuwa nimepata nafuu sana hata daktari akaniruhusu kuketi. Katika siku chache nilikuwa mzima.” Vema, akasema... Kasema, “Loo, Bwana asifiwe!” Akasema, “Mwanangu, unapaswa kuninii...”

⁷¹ Akasema, “Mama, unaanza kutenda kama watu hao.” Kasema, “Sikiliza, mama.” Kasema, “Tumejifunza huko shuleni ya kwamba mahali hapo aliposoma, Maandiko ya pili aliyosoma yalikuwa katika Marko 16, ambapo, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya.’” Kasema, “Tulijifunza huko shuleni ya kwamba Marko 16, kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa.” Kasema, “Unaona, watu hao hawaendi shuleni, karibu wote kule chini. Hawana elimu, kwa namna fulani ni watu wasiojua kusoma.” Kasema, “Wa—wana nia nzuri, hapana shaka.” Lakini kasema, “Tulijifunza shuleni ya kwamba, kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, hivyo viliongezwa tu, labda na Vatikani ama wowote wale, lakini,” kasema, “sababu ni kwamba sehemu hiyo haijavuviwa.”

⁷² Maskini mama huyu akapiga mayowe makubwa ya, “Haleluya!” Na kwa hiyo akasema . . .

Akasema, “Mama! Vema, ni kitu gani kinachokufanya useme hivyo?”

⁷³ Akasema, “Nilikuwa tu nikiwazia, mwanangu, kama Mungu angeweza kuniponya kwa Neno lisilovuviwa, kweli angefanya nini hasa na Lile lililovuviwa?”

⁷⁴ Kwa hiyo—kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo na ahadi zingine. “Ombeni lolote katika Jina Langu, nami nitalifanya.” “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” “Mnapoomba, aminini mnapokea mliyoomba, nanyi mtapewa.” Mnaona, yote yametiwa pumzi, kila sehemu yake.

⁷⁵ Wakati Morris Reidhead, mwanazuoni hodari sana, alipokuja nyumbani kwangu. Alipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu; akaanguka juu ya meza ndogo ya kahawa hapo nyumbani. Akaniambia, kasema, “Ndugu Branham, ninasikia ya kwamba wewe ulikuwa ni—ninii . . . Wewe ni Mbaptisti.”

⁷⁶ Nami nikasema, “Vema, niliwekwa tu wakfu kuwa mhudumu, kanisa la Kimishenari la Kibaptisti, nikiwa mvulana; mimi si mfuasi wa ninii . . .”

⁷⁷ Kasema, “Vema, hawa Wapentekoste unaoshikamana nao kotekote ni akina nani?”

Nikasema, “Hao ni watu tu kama mimi na wewe.”

⁷⁸ Akasema. “Vema, sikiliza,” kasema, “je! unafikiri huyo waliyempata ni Roho Mtakatifu?”

Nikasema, “Hakika.”

Akasema, “Kwa nini huku kutupa mateke kote na kuchapua miguu na kupaza sauti?”

⁷⁹ Nikasema, “Vema, hawana budi kutoa mvuke kutoka kwenye filimbi. Kama hawaitumii, kuyafanya magurudumu

yazunguke.” Nikasema, “Wewe wafanye—wafanye tu kujifunza yote kuhusiana nayo, badala ya kuilipua itoke namna hiyo. Iingize kazini, imani, huko nje mtaani, ukijaribu kuwaingiza watu, katika Ufalme wa Mungu.”

⁸⁰ Naye akasema, “Vema, nimewaona wakifanya hayo yote.” Kasema, “Nitakwambia ni kwa nini niko hapa.” Kasema, “Mvulana mzuri kutoka India,” kasema, “alipata elimu yake na kisomo.” Kasema, “Mimi, nilipoenda likizo, kumpeleka kwenye ndege, kumpandisha kwenye ndege, kumsindikiza arudi katika nchi za ng’ambo, nilimwambia, nikasema, ‘Mwanangu, sasa una elimu yako, unarudi kwa watu wako. . .’” Nafikiri alisomea. . . Mimi sininii. . . nafikiri elektroniki.

⁸¹ Basi akasema, kasema, wakati alipoanza kurudi, alimwambia, “Mbona usininii. . . usimwache huyo nabii wa kale aliyekufa, Muhammed, na umpate Yesu Kristo halisi aliyefufuka moyoni mwako?”

Naye akasema, “Bwana, ninataka kukuuliza jambo fulani.”

⁸² Sasa kumbukeni, hii ni kutoka moja ya shule kubwa sana za Biblia, shule za kimsingi, mtu huyu alikuwa mmoja wa walimu wao.

⁸³ Akasema, “Yesu wako angeweza kunifanyia nini zaidi ya yale nabii wangu anayoweza kufanya?”

⁸⁴ Akasema, “Vema,” akasema, “Yesu wangu anaweza kukupa Uzima wa Milele.”

⁸⁵ Akasema, “Jamani, Kurani inaahidi jambo lilo hilo.” Kurani ni Biblia ya Waislamu, mwajua. Kasema, “Inaahidi jambo lilo hilo.”

Kasema, “Vema,” akasema, “naam, mimi. . .”

⁸⁶ Kasema, “Unajua, Kurani haikuahidi chochote. Muhammed hakuahidi kitu ila—ila uzima baada ya mauti.” Kasema, “Yesu aliwaahidi ninyi walimu, ya kwamba, ‘Ishara hizi na maajabu yangewafuata.’” Kasema, “Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.” Naye akasema, “Tunangojea kuona jambo hilo likifanywa, kuwaona nyinyi walimu mkifanya jambo hilo.” Wazia jambo hilo!

⁸⁷ Akaniambia, “Papo hapo,” akasema, “nilitambua sikuwa nimekutana na mvulana wa kupiga dharuba moja. Na ninamjua. . . Mtu aliyejua aliyokuwa akinena habari zake.” Huenda alichonganisha. Lakini hiyo ndiyo njia nzuri ya kufanya jambo hilo, kuachilia adui akurukie wakati mmoja namna hiyo halafu mtu hujui uende wapi. Unaona? Kwa hiyo na akasema, “Nilitambua basi huyo hakuwa mvulana wa kupiga dharuba moja.”

⁸⁸ Naye akasema—akasema, “Vema, sasa angalia hapa. Yesu amefufuka katika wafu.”

⁸⁹ Akasema, “Ati amefufuka?” Kasema, “Mmekuwa na miaka elfu mbili ya kuthibitisha jambo hilo, na angalau thuluthi mbili za dunia hazijasikia habari Zake kamwe. Sasa ninyi watu mna shida gani?” Akasema, “Hebu Muhammed na afufuke katika wafu, na ulimwengu mzima utajua jambo hilo katika masaa ishirini na manne.” Na hiyo ni kweli.

⁹⁰ Unaona, wana farasi anayesimama kaburini pake. Nimemwona pale. Wanabadilishana walinzi kila kama baada ya saa nne, bado, wakimtarajia kufufuka. Pale katika mfano, akija juu ya farasi mweupe, mnaona, apate kuuteka ulimwengu.

⁹¹ Na kwa hiyo akasema, “Hebu—hebu na afufuke katika wafu, na ulimwengu wote utajua habari hizo.”

⁹² Akasema, “Vema, Yesu alifufuka katika wafu.” Akasema, “Nabii wenu yuko kaburini.”

Akasema, “Unajuaje alifufuka katika wafu?”

Mwalimu akasema, “Yeye yuko moyoni mwangu.”

Akasema, “Mohammed yuko moyoni mwangu, pia, bwana.”

Akasema, “Lakini nina furaha na amani.”

⁹³ Akasema, “Bwana, Uislamu unaweza kusababisha saikolojia kadiri Ukristo unavyoweza.” Na wao hufanya hivyo. Unapaswa kuwasikia wakipaza sauti na kupiga mayowe. Hiyo ni kweli. “Kudhihirisha saikolojia vile vile kadiri ambavyo Ukristo uwezavyo.” Akasema, “Vema, unamaanisha nini wakati uliposema ya kwamba Yesu aliwaahidi mambo haya yote?” Kasema, “Nafikiri unarejea kwenye Marko 16?”

Akasema, “Ndiyo, hiyo ni mojawapo. Si hapo tu, bali hiyo ni mojawapo.”

⁹⁴ “Yesu alisema, Maneno ya mwisho aliyoliambia Kanisa Lake, ‘Enendeni ulimwenguni kote, unaona, mkaihubiri Injili, na ishara hizi zitafuatana na aminiye.’ Umbali gani? ‘Ulimwenguni kote; kwa kila kiumbe. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.’ Maneno ya mwisho aliyosema, kulingana na Maandiko yenu.”

⁹⁵ Akasema, “Vema, unaona,” kasema, “hiyo ni ninii tu...” Kasema, “Unaona, sehemu hiyo haijatiwa pumzi.” Kasema, “Yeye kweli hakumaanisha jambo hilo. Hilo halikuwa...”

⁹⁶ Akasema, “Ati haijavuviwa?” Kasema, “Mnasoma Kitabu cha aina gani?” Kasema, “Kurani nzima imevuviwa.” Boo! Ni kushindwa kwa udhaifu wa theolojia, theolojia ya kujibunia ambayo haina Ro—Roho wa kusimama na kukabiliana na jambo hilo.

⁹⁷ Kama vile wale wana wa Kiebrania walivyosema, “Mungu wetu anaweza kutuokoa kutoka kwenye tanuru hili la moto, lakini hata hivyo hatutaisujudu sanamu hii.” Tunahitaji watu wenye ujasiri. Watu ambao wamemwamini Mungu daima

wamekuwa wajasiri na kuamini katika mambo ya kimbinguni. Watu wanaomwamini Mungu!

⁹⁸ Bw. Reidhead akasema, “Nilipiga mguu sakafuni, Ndugu Branham, nikakung’uta mavumbi namna *hiyo*, wala nisingeweza kumjibu mtu huyo.” Akasema, “Nilikusudia moyoni mwangu kuja kukuona baada ya hayo, na nikuulize maana ya haya yote.” Kisha kasema, “Mimi hapa.” Akasema, “Kama Roho Mtakatifu. . .”

⁹⁹ Kasema, “Ndugu Branham, mama yangu alinipeleka shuleni.” Kisha akasema, “Mimi, nilipopata BA yangu, nilifikiri hivyo ndivyo hasa. . .”

Nikasema, “Ninajua unalomaanisha.”

¹⁰⁰ Kasema, “Ndipo siku moja nikapata BA yangu, nikafikiri papo hapo nitampata Kristo. Hakuwapo wakati nilipopata Digrii yangu ya Udaktari.” Kasema, “Nina digrii za kutosha, digrii za heshima, za kutosha kukandika kuta zako, basi Kristo yuko wapi katika haya yote?”

¹⁰¹ Nikasema, “Mimi ni nani kusema ya kwamba hao walimu wamekosea? Lakini hilo silo tunalonena habari zake. Ni ule Utu, Kristo, ambaye huna budi kumjua.”

¹⁰² Sasa mtu huyo anafanya miamsho mikubwa kila mahali. Na Daktari Lee Vayle pale, rafiki msiri wangu, ni rafiki yake, pia. Naye anapata mafanikio makubwa, akiwaombea wagonjwa na kufanya mikutano mikubwa mno na kila kitu. Ni kwa sababu mtu huyo aliamini.

¹⁰³ Sasa, unaona, Roho aliyekuwa ndani ya Kristo, ule mwili, Yesu ambaye alikuwa ni Mungu, Imanueli. Roho Mtakatifu, Mungu, alishuka katika Kristo, Naye akafanyika “Mungu pamoja nasi.” Halafu Yeye alikuwa. . . Huyo alikuwa atukomoe; Damu Yake ilimwagika.

¹⁰⁴ Sasa, katika Agano la Kale, wakati mwabuduo alipokuja na kuweka mikono yake juu ya dhabihu yake, na akakata koo la. . . kuhani alilikata, ama alitoa dhabihu. Mwabuduo aliishika dhabibu kwa mikono yake, na kuhisi ninii—kuchinjwa, na maskini mwana-kondoo huyo akifa; maskini sufu yake ikilowa kwa damu yake, kote kwenye mikono ya mwaminio, na kadhalika, imetekwa kwenye sinia, ipate kuchomwa pale juu ya madhabahu. Mwaminio alitambua ya kwamba alipaswa awe ndiye anayekufa kwa ajili ya dhambi hiyo, bali mwana-kondoo alikuwa anakufa mahali pake. Sasa, lakini uhai uliokuwa katika damu hiyo, usingeweza kumrudia mwabuduo, kwa sababu ilikuwa ni damu ya mnyama, ambaye hana nafsi. Lakini katika. . . Kwa hiyo kulikuwa na kumbukumbu la dhambi, daima.

¹⁰⁵ Lakini, sasa, Yesu akiwa ni Imanueli, basi Uhai wa Mungu ulikuwa ndani Yake, na huo hurudi; si Uhai wa mwanadamu

tu, bali Mungu Mwenyewe, katika umbo la Roho Mtakatifu, anarudi na kuwafanya ninyi wana na binti za Mungu. Ndipo ninyi ni wana na binti. Na basi wakati unapoonza adha na mateso na adhabu ambazo Yesu alipitia, akadhihakiwa, huduma Yake ikaitwa kazi ya ibilisi, “Beelzebuli,” na kudhihakiwa, na kudharauliwa, na viongozi wa dini, na kukataliwa. “Alikuwa kwa Walio Wake; walio Wake hawakumpokea.” Na mambo aliyopitia! Halafu ikambidi kutoa uhai Wake kama dhabihu msalabani, kuwakomboa wale ambao Mungu alikuwa ametangulia kuwajua. Kuwakomboa; kuwarudisha mahali ambapo wa—walianguka. Ndipo, Mungu alifanya jambo hilo kusudi apate kumtuma tena Roho Mtakatifu juu ya Kanisa sasa, ili kwamba lininii . . . watu, waaminio. Ni kwa ajili ya waaminio peke yao.

¹⁰⁶ Si kwa ajili ya wasioamini. Wao kamwe hawataliona. Wamekufa, kwanza.

¹⁰⁷ Angalia hao Mafarisayo walipomwona Yesu akifanya ishara ile ile ambayo ilikusudiwa kuwa ndiyo ishara ya Masihi.

¹⁰⁸ Mwangelie Petro, yeye aliamini wakati uo huo. Na Nathanaeli aliamini papo hapo. Yule mwanamke kisimani aliamini; kipofu Batimayo. Wote hao walioipokea, waliamini.

¹⁰⁹ Lakini hao viongozi walisimama pale na kusema; “Ni Beelzebuli, roho mchafu, namna fulani ya mzaha ama ujanja.”

¹¹⁰ Yesu alisema, “Mkisema hivyo dhidi Yangu, nitawasamehe,” ile dhabihu haikuwa imetolewa, “bali Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu wala katika ulimwengu ujao.”

¹¹¹ Ni kwa nini wao hawakuweza kuiamini? Yesu alisema “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mtazifanya.” Hiyo ni kweli.

¹¹² Kuamini Neno, ni kulipokea Neno na kuliruhusu liwe Hai. Sasa, Mungu akionyesha pale jinsi alivyokuwa akithibitisha agano hili. Inapaswa kuwa hivyo. Kanisa! Si shirika, si madhehebu; bali ni mtu binafsi pamoja na Mungu yabidi wawe ni Roho yule yule. Hilo ndilo kusudi la Mungu, hapo mwanzo.

¹¹³ Adamu na Hawa walikuwa ni roho yule yule. Biblia ilisema katika Mwanzo, katika 1:27, “Kwa mfano wa Mungu . . .” Mungu ni Roho. “Kwa mfano wa Mungu alimwumba; mwanamume na mwanamke aliwumba,” katika umbo la roho iliyokuwa ndani ya Mungu. Na Adamu alipaswa kuishughulikia a—ardhi, kama vile tu Roho Mtakatifu anavyopaswa kuliongoza Kanisa sasa. Na, hata hivyo, mtu hakuwa katika mwili, naye alikuwa vyote viwili wa kiume na pia alikuwa wa kike, kwa sababu ni roho yule yule.

¹¹⁴ Ndipo Mungu akamwumba mtu toka kwenye mavumbi ya ardhi, na kumfanya katika umbo la mnyama. Ambapo, sisi sasa ni mnyama, tunajua. Sisi ni—sisi ni mamalia. Na hao ni wanyama

wenye damu yenye joto, nasi tuko katika mfano huo wa uhai wa mnyama.

¹¹⁵ Na ndipo Mungu akachukua ubavu toka kwa Adamu, si ninii. . . Mwanamke ni zaotuka la mwanamume, hakuwa hasa katika uumbaji wa asili. Yeye alichukua ubavu. Aliutenganisha mwili, kisha akachukua roho ya kike kutoka kwa Adamu na kuiweka katika Hawa. Huyu hapo mwanamume na mwanamke.

¹¹⁶ Na wakati wanapotoka kwenye nafasi hizo, wako nje ya hali yao sahihi. Kuna upotovu mahali fulani. Wakati mwanamke anapotaka kuwa wa kiume, ama mwa—ama mwa—ama mwamamume anataka kufanya kama wa kike, kuna kasoro fulani mahali fulani. Wako nje ya hali yao halisi.

¹¹⁷ Tunaona hilo katika Rebeka na—na Isaka, wakiwa ni wa ukoo mmoja damu yao, unaona, lakini sasa hilo lilikuwa ni kufananisha uzao wa kawaida wa Israeli. Lakini, kwa imani, Kristo alijitokeza jukwaani, ambapo si katika mambo ya kawaida.

¹¹⁸ Kama vile ishara ilivyokuwa, ile damu kwenye mwimo wa mlango, kule chini Misri. Haidhuru walitahiriwaje, walikuwa na agano jinsi gani, ile ishara ilipaswa kuonyeshwa la sivyo lile agano lilibatilishwa. Hakika. “Nitakapoiona damu, nitapita juu yenu.”

¹¹⁹ Sasa ile ishara siyo Damu; ni ule Uhai uliokuwa katika hiyo Damu, Roho Mtakatifu. Na hiyo ni. . . Sijali wewe ni wa kidini jinsi gani; isipokuwa uwe umempokea Roho Mtakatifu, utaangamia. Hiyo ndiyo njia pekee. Hakuna Andiko lingine la kufanya lolote, ila hilo tu. “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Waefeso 4:30.

¹²⁰ Angalia sasa, tunarudi, na hiyo inaonyesha ya kwamba Adamu na Hawa walikuwa ni mmoja, kwanza. Mume na mke wangali wanapaswa kuwa ni mmoja.

¹²¹ Sasa, lakini wakati walipotenganishwa, wakati huo, kimwili, hapo ndipo Hawa alipoanguka. Akaanguka! Kwa nini? Kwa kutokuamini Neno, kila sehemu Yake. Watu wengine wanaweza kuchukua sehemu moja ya Neno, bali si zingine zote. Inabidi lote liwepo. Unaona? Unaona? Yeye alitilia shaka tu sehemu Yake moja. Na kama magonjwa haya yote na shida ambazo tumekuwa nazo sasa zilitokana na mwanamke mmoja kutilia shaka sehemu Yake moja, tutarudishiwa chochote pungufu ya kuliadini lote, na kulikubali lote? Hiyo ilikuwa ninii yao. . . Walikingwa na Neno hilo. Walipotenganishwa, katika mwili, walianguka. Mwanamke alianguka, kwa Neno. Yeye. . . Angalia, alitafuta kitu gani?

¹²² Hakika watu wengi sana siku hizi, wanatamani njia bora zaidi, ya kimtindo, njia rahisi. Hawataki kukabiliana na kitu

kilichowekwa mbele zao. Wakifanya hivyo, wanafukuzwa katika dhehebu lao, wanatengwa, hawajaliwi.

¹²³ Hivi hamjui, ya kwamba, “Watu wote watawanenea vibaya, kwa uongo, kwa ajili Yangu. Furahini na kushangilia sana, kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa Mbinguni, kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. Na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.”

¹²⁴ Sasa tunamtaka aseme nini tena? Tungesema maelfu ya Maneno, Maandiko, yanayohusu jambo hilo, yangetoka Mwanzo mpaka Ufunuo.

¹²⁵ Ni kwamba chochote tulicho nacho siku hizi, kilianza katika Mwanzo. Ndio mlango wa mbegu. Kutokuamini kote na kila kitu kilianza papa hapa. Kanisa lilianza pale pale. Kila kitu kilianza pale. Ni kama mizabibu miwili ikikua, na mmoja ukiigiza huo mwingine, na ukikua mpaka karibu unafanana.

¹²⁶ Ni kama Moabu na Musa pia. Hao hapo Israeli wanakuja, wachache, hawana madhehebu, si taifa hata. Nao walikuwa na dhabihu ile ile hapa katika Moabu; dhehebu zuri, wakuu wao wote walitoka, na kutoa dhabihu ile ile. Wakijaribu kuninii . . . Askofu wao kule, Balaamu, alishuka akaja kulaani kile Mungu alichobariki. Waliwaza, “Watu hawa mahaini! Hata hawana kanisa la nyumbani, tuseme. Ni wazururaji tu.”

¹²⁷ Naye akasema, “Bali walishindwa kusikia kule kupaza sauti kwa Mfalme kambini. Alishindwa kuona ule uponyaji wa Kiungu ukiingia pale, kwa yule nyoka. Na ule Mwamba uliopigwa, upate kuwapa uzima! Ukelele wa Mfalme kambini!”

¹²⁸ Yeye alishindwa kuona jambo Hilo, huyo askofu kipofu. Lakini hata hivyo, kimsingi, alikuwa sahihi tu kama Musa alivyokuwa; madhabahu saba, dhabihu saba, hata alitoa dhabihu ya kondoo mume, ikinena juu ya kuja kwa Kristo.

¹²⁹ Lakini Mungu hahitaji mtu yeyote kumfasiri. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Yeye huweka ahadi, halafu anaitimiza, na hiyo ndiyo fasiri yake. Hakuna mtu anayepaswa kulifasiri. Mungu hamwambii mtu yeyote aifasiri. “Biblia si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote.” Kila mtu akijaribu kusema inamaanisha *hivi, vile*. Acha Mungu ajinenee Mwenyewe. Yeye Ndiye anayejifasiria. Aliweka ahadi; anasimama nyuma yake. Anafanya hivyo, kwa waaminio.

¹³⁰ Lakini wasioamini hawapokei chochote. Si kwa ajili yao. Wamekufa, kwanza. Hata hawakupata kuwakilishwa kamwe. Hamna kitu ndani yao. Wao ni maganda yaliyokufa. Hutaki kuwa namna hiyo.

“Jazweni na Roho!”

¹³¹ Angalia, Yeye aliwatenganisha Hawa na Adamu, naye Hawa akaanguka. Adamu aliambatana naye. Sasa, “Adamu

hakudanganywa.” Hawa alidanganywa. Lakini Adamu, Adamu wa kwanza, alikuwa ni mwana wa Mungu pia. Naye alitoka nje kwa sababu ya kumpenda Hawa, kujaribu kumrudisha, maana yeye alimpenda.

¹³² Kristo alifanya jambo lile lile, kumkomboa arudi. Kwenye nini? Kwenye Neno. Ni kitu gani kilichosababisha kule kuanguka? Neno, kutokuamini Neno, Neno lote. Naye Kristo alikuja apate kuwa mmoja wetu, Uhai Wake ndani yetu, apate kuliendeleza Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mungu yule yule! Hiyo ndiyo sababu Yeye alikuja, apate kufanya jambo hilo.

¹³³ Sasa tunaona, katika kule kuthibitishwa, kutukomboa kuturejesha Kwake, kuwakomboa watoto wakaidi waliopotea katika nyumba hizi za maiti; na kurudi kwenye Neno tena, kurudi kwenye Neno lililotambulishwa!

¹³⁴ Sasa hao Wayahudi, wakati Yesu alipokuja, wangeweza kusema, “Tuna Neno. Tuna Neno. *Hivi* ndivyo Musa alivyosema. Sisi ni wanafunzi wa Musa.” Yesu, akiwa tu na umri wa miaka kumi na miwili, akishindana nao. Ndipo wakati... Unaona, hivyo ndivyo mwanadamu anavyolifanyia.

¹³⁵ Lakini Yesu alisema, “Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Kwa kuwa, kazi alizonipa Baba kufanya, zinashuhudia kwamba Mimi ni Nani.”

¹³⁶ Nani? Mtu ye yote aliyetumwa na Mungu, Mungu huzishuhudia kazi ambazo amemkusudia yeye kufanya. Kama hashuhudii, Maandiko hayaziungi mkono, ziache.

¹³⁷ Hata katika Agano la Kale, walikuwa na njia ya kujua kama ni kweli ama si kweli. Waliwapeleka huko, mwotaji, ama—ama mtabiri, ama yeyote yule, waliwapeleka kwenye Urimu Thumimu. Hiyo ilikuwa ni Nuru ya kimbinguni.

¹³⁸ Mungu daima ni wa kimbinguni, anafanya kazi katika mambo ya kimbinguni. Mradi kuna Mungu pale, kuna ya kimbinguni, kama ni Yehova Mungu.

¹³⁹ Na, wakati, haidhuru hiyo ndoto inasikika ni nzuri jinsi gani, kama haikuakisi kwenye hiyo Urimu Thumimu, basi ilikuwa si kweli.

¹⁴⁰ Sasa ule ukuhani wa kale wa Haruni umeondolewa, bali tungali tuna Urimu Thumimu. Huu ni ufunuo wa Yesu Kristo, unamfunua katika Neno hili. Na chochote ambacho ni kinyume cha Neno hilo si Mungu; kinacholipinga. Lakini Mungu hujinenea Mwenyewe. Anajitambulisha Mwenyewe kwa Neno Lake.

Hapo ndipo Yesu alipomshindia Shetani. “Imeandikwa...”

¹⁴¹ Ndipo huyu hapa Shetani anarudi, na akaanguka kwa kishindo tena. Akasema, “Naam, imeandikwa pia...” Lakini wakati huo, wakati alipokuja, aligonga vo—volteji kubwa. Wakati huo iliunguza mbawa zake. Aliruka akatoka hapo, basi.

¹⁴² Akasema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’ Rudi nyuma Yangu, Shetani!” Mnaona?

¹⁴³ Angalia yaliyotukia. Mungu daima amejitambulisha Mwenyewe kwa Neno Lake lililoahidiwa. Sasa kama hao Mafarisayo wangelikuwa wameangalia moja kwa moja huko nyuma, Musa alisema, “Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Hayo yalikuwa yako kwenye Maandiko.

¹⁴⁴ Lakini si ajabu Yesu alimshukuru Baba, kasema, “Nakushukuru Wewe, Baba, umeficha jambo Hili kwa macho ya wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga ambao wataweza kujifunza.”

¹⁴⁵ Wakati alipomwambia Petro kwenye siku ile, wakati waliposhuka wakaja. Wakati aliposema, “Watu husema kwamba Mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

¹⁴⁶ “Mmoja wao alisema Wewe ni ‘Eliya,’ na mmoja alisema Wewe ni ‘Musa,’ na kadhalika.”

Akasema, “Lakini hilo swali. Niliwauliza nyinyi.”

Kasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

¹⁴⁷ Akasema, “Heri wewe Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili. Kamwe hukujifunza hili kwenye seminari, hakuna mtu aliyekufundisha hili, bali ni ufunuo.” Loo, jamani! “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda,” ule ufunuo, ama utambulisho wa Yesu Kristo.

Akasema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini.”

¹⁴⁸ Sasa hebu na tuendeleo na safari. Tunamkuta... Sasa hebu na twende kwenye mlango wa 17. Tunamwona hapa katika mlango wa 17, mahali alipomtokea Ibrahimu baada ya thibitisho la jambo hili, akionyesha vile atakavyofanya.

¹⁴⁹ Na sasa, kumbukeni, Roho huja juu ya... Na Roho aliye Kanisani, Kanisa halisi, Kanisa la kweli, Kanisa la Mungu, watu wa Mungu; Roho aliye ndani yao, yumo, Roho yeye yule yuko juu ya Kristo, pamoja na ahadi, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

¹⁵⁰ Kumbukeni, wakati mmoja katika kule kusulubishwa, kabla tu ya kusulubishwa, walimfunga tambara usoni Mwake, na kumpiga kichwani, kwa tete, kasema, “Sasa kama Wewe ni Mwana wa Mungu, hilo... Wewe ni—Wewe ni nabii,

wananiambia. Tabiri, nabii!” Wakapitishiana hiyo fimbo, “Twambie ni nani aliyekupiga.” Mnamwona huyo ibilisi? Mnamwona?

¹⁵¹ Akasema, “Nasikia ya kwamba Wewe ni mfanya miujiza mashuhuri. Geuza mawe haya yawe mkate. Hebu nikuone ukifanya jambo hilo. Nita—nita—nitakuamini kama utafanya jambo hilo namna hiyo, kuyageuza mawe haya kuwa mkate. Nitaamini. Nitaafanya hivyo.”

¹⁵² Mtu fulani aliniambia si muda mrefu ulopita, kasema, “Kama unaweza kutoa mtu mmoja ambaye ameponywa, pamoja na taarifa ya daktari!”

¹⁵³ Nikasema, “Loo, rehema, jamani, nyamaza. Salala!” Nikasema, “Nitakuletea madaktari kwa mamia.”

Akasema, “Nina dola elfu moja zinazokungojea, kama ukiwaleta.”

¹⁵⁴ Ndipo nikawaleta madaktari, pamoja na hao wagonjwa. Akasema, “Vema, hizo pesa ziko katika . . .”

¹⁵⁵ Nikasema, “Ninataka pesa hizo kwa ajili ya matoleo ya kimishenari.” Naye akasema . . . “Kumtuma mtu anayeamini Injili, nchi za ng’ambo.”

¹⁵⁶ Akasema, “Vema, hebu nimchukue msichana mdogo, na mimi na ndugu zangu tusimame hapo, nasi tutakata mkono wake, na halafu wewe uuponye papa hapa mbele zetu, nasi tutakuamini.”

¹⁵⁷ Nikasema, “Unahitaji uponyaji wa akili.” Hiyo ni kweli kabisa. Mtu aliyepagawa namna hiyo na ibilisi!

¹⁵⁸ Yeye yule aliyesema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, kama Wewe ndiwe, shuka kutoka msalabani.” Loo, wakati Biblia yenyewe ilisema ilimbidi kutundikwa msalabani!

¹⁵⁹ Kayafa alisema, “Aliwaokoa wengine; hawezi kujiokoa Mwenyewe.” Bila kujua ya kwamba hiyo, si kitu kingine bali ndiyo sifa kubwa sana aliyopata kupewa. Kama angalijiokoa, asingeweza kuwaokoa wengine. Ilimbidi kujitoa.

¹⁶⁰ Hakika, Yeye alijua ni nani aliyempiga, bali Yeye hamfanyii ibilisi vitimbi. Mungu si mfurahishaji. Yeye hamfanyii ibilisi vichekesho. Kazi Zake zinatuma kwa wale wanaoamini, si zikafanyiwe vitimbi.

¹⁶¹ Angalia, Yeye alimtokea hapa wakati alipokuwa na umri wa miaka tisini na tisa, Naye alimtokea katika jina la Mwenyezi Mungu. Jina hilo hapo, katika Kiebrania, ni *El Shaddai*.

¹⁶² Sasa, Mungu ana majina saba ambatani, ya ukombozi. Tunajua jambo hilo. Wala huwezi kuyatenganisha na Kristo. Huwezi kuyatenganisha. Kristo alitimiza kila moja ya majina hayo ambatani, majina ya ukombozi. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye, je! mnaamini Yeye

ni Yehova-Yire, “sadaka iliyoandaliwa na Bwana”? [“Amina.”] Basi vipi kuhusu *Yehova-Rafa*, “Bwana huyaponya magonjwa yako yote”? [“Amina.”] Na kama hayo hayakutumiwa kwa Kristo, basi Yeye hakuwa Yehova-Yire. Kwa hiyo huwezi kuyatenganisha, jambo hilo lote limefunganishwa, na hivyo ndivyo ilivyo. Yeye hawezi kuwa Yehova-Rafa bila ya kuwa Yehova-Yire, wala hawezi kuwa Yehova-Yire bila ya kuwa Yehova-Rafa. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.” Hakuna ubishi juu ya Hilo.

¹⁶³ Sasa tunaona hapa, Yeye anajitokeza katika jina la *El Shaddai*, “Mwenyezi.” Ninii... Kwa kweli, neno hilo, neno la Kiebrania *shad*, s-h-a-d, wengine wanalitamka “shade.” *Shad* linamaanisha “ziwa,” kama ziwa la mwanamke. Naye alimtokea katika jina la *El Shaddai*, ambalo liko katika wingi, *mwenye maziwa*. “Mimi ni Mungu Mwenye Maziwa. Ibrahimu, mwenye umri wa miaka tisini na tisa, tembea mbele Zangu! Uwe mkamilifu, amini Neno Langu! Endelea tu kuamini! Niliahidi, ukiwa na miaka sabini na mitano; hili hapa, imekuwa—imekuwa ni miaka ishirini na minne sasa tangu nilipokupa hiyo ahadi.” Na ni fa—faraja ya jinsi gani ingepaswa kuwa kwa mwanamume mzee, mwenye umri wa miaka tisini na tisa. Na nguvu zake zote zimekwisha, na hapa Mungu anasimama mbele Zake, kasema, “Mimi ni *El Shaddai*. Mimi ni Mungu Mwenye Maziwa.” Amina. “Nyonya nguvu zako toka Kwangu. Mimi ni nguvu zako.”

¹⁶⁴ Kama vile, kama Agano Jipya na Agano la Kale, Mungu Mwenye Maziwa. “Mimi ni Mungu Mwenye Maziwa, nyonya nguvu zako kutoka Kwangu.”

¹⁶⁵ Ni kama vile mtoto mchanga wakati ni mgonjwa, anasumbuka; mgonjwa, dhaifu, anaegemea kwenye ziwa la mama yake na kunyonya arejeshe nguvu zake kutoka kwa mama. Kwa maneno mengine, “Ibrahimu, wewe si kitu ila ni mtoto mchanga Kwangu.” Umri wa miaka tisini na tisa, haujawa ni muda hata kidogo, maisha yake.

¹⁶⁶ Kumbukeni tu, Yesu alisulubishwa, kama jana. Miaka elfu moja duniani—duniani, ni siku moja tu kwa Mungu. Unaona, ni kama tu alisulubishwa jana.

¹⁶⁷ Pia angalia, “Mimi ni *El Shaddai*. Wewe ni mtoto mchanga, dhaifu. Lakini egemea kifuani mwangu, ahadi Yangu, na unyonye toka Kwangu upate nguvu zako. Mimi ni muumba niliyetundika mbingu na nchi, nikaweka nyota huko juu. Je! kuna jambo lililo kuu sana kwa Mungu? Mimi ni *El Shaddai*, nawe ni mtoto Wangu. Ingawa wewe ni dhaifu, nami ninakuachilia uwe namna hiyo nipate tu kuona vile utakavyofanya juu ya jambo hilo. Nitatoa mfano kwa watu wajao, kusudi binadamu waliamini neno Langu. Nitalitimiza. Haidhuru itagharimu nini, itachukua muda gani, nitalifanya. Nitalitimiza. *El Shaddai*! Nyonya nguvu zako toka Kwangu.”

Loo, unasema, “Laiti ningaliweza kuamini . . .”

¹⁶⁸ Yeye angali ni El Shaddai. Yeye angali ni Mungu Mwenye Maziwa, Agano Jipya na la Kale. Nyonya tu nguvu zako toka Kwake, loo, kila kitu unachohitaji. Mtoto mchanga, ni dhaifu, inambidi kunyonya nguvu zake toka kwa mama yake; hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kupata nguvu zake. Hiyo ndiyo njia pekee mwaminio anayoweza kupata nguvu zake, ni kuzinyonya toka kwenye Neno la Mungu. Hizo ndizo nguvu zake, ahadi za Mungu kwake. Simama hapa na uliamini!

¹⁶⁹ Na si kwamba tu mtoto huyo mchanga amewakilishwa hapa wakati ni mgonjwa, akisumbuka, mama anaweza kumpa ziwa la—lake, naye anaanza kunyonya arejeshe nguvu zake; anashiba wakati akinyonya.

¹⁷⁰ Hivyo ndivyo ilivyo kwa mtoto halisi wa Mungu. Haidhuru mwenye kushuku anasemaje, lolote analoamini. Kama kweli unaamini, Yesu hawezi kusema uongo. Umeridhika ya kwamba umefunuliwa jambo Hilo. Unayo ahadi, wala hakuna kitu kitakachoikomesha. “Juu ya mwamba huu nalijenga Kanisa Langu,” unaona, Neno la Kweli, la kiroho, lililofunuliwa.

¹⁷¹ Wakati ukingoja, ukipumzika katika imani yako, chukua ahadi ya Mungu. “Ninakuamini, Bwana. Uliahidi kunipa ubatizo wa Roho. Ninapumzika katika ninii Yako . . . katika imani. Imani yangu niliyo nayo Kwako, ninanyonya toka kwenye nguvu zangu, nipate riziki yangu, kutoka—kutoka . . . kwa ajili ya afya yangu, kutoka kwenye chemchemi Yako, Neno.

¹⁷² “Mtu huyo hataishi kwa mkate tu, bali kutoka kifua mwa Mungu atanyonya nguvu zake.” Kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu, atapata nguvu zake Yeye anapotoka katika kinywa—kinywa cha Mungu, Neno.

¹⁷³ Kama vile Ibrahimu, Ibrahimu alikuwa akipumzika. Sasa alikuwa ameishi na Sara tangu alipokuwa msichana m—mdogo. Alikuwa ni dada yake wa kambo, naye alikuwa akiishi naye na akamwoa. Na, yeye, alikwisha kuwa . . . Alikuwa tasa. Hakuwa na watoto. Naye huyu hapa sasa, tayari yeye. . . kama yeye ana tisini. . . tisini na tisa. Mkewe ana themanini na tisa, umri wa miaka themanini na tisa. “Lakini, Ibrahimu, pumzika katika imani ya Neno Langu. Nitakuahidi, nitafanya jambo hilo. Mimi ni El Shaddai. Mimi ni Mungu Mwenye Maziwa kwa ajili ya watoto Wangu wanaoamini.” Kama hutaki kunyonya, vema, basi usiseme lolote juu ya jambo hilo, unaona. Lakini kama wewe ni mtoto, unanyonya, unapumzika, kila ahadi!

¹⁷⁴ Angalia, imani halisi inatulia juu ya mwamba imara wa ahadi ya Neno la Mungu. Haitikisiki. Imani halisi imetia nanga.

¹⁷⁵ Kama vile kwa nyota ya kaskazini, nyota ya kaskazini ndiyo nguzo ya kujifunga kwayo kwa kila nahodha, dira humwelekeza kwenye nyota hiyo ya kaskazini tu. Naye Mungu, Neno, ndilo nyota ya kaskazini ya kila Mkristo, kama umepotea, naye Roho

Mtakatifu ndiye anayekuelekeza Kwake. Hataelekeza kwenye kitu kingine chochote. Itikadi nyingine zote, na kadhalika, na—na Ukristo uliochanganyikana nazo, iwe ni chochote kile; ni kama ulimwengu, ukisogea, unabadilisha hizo nyota, bali hauwezi kubadilisha nyota ya kaskazini. Wala hakuna chochote kinachoweza kulibadilisha Neno la Mungu. Jitie nanga Kwake, kaa Nalo!

¹⁷⁶ Sasa, imani halisi haisogezwi na kanuni za imani na mafundisho ya kujibunia ya wanadamu, na kutokuamini. Inadumu moja kwa moja na Neno, imani halisi katika Neno.

¹⁷⁷ Nawe unaweza kuweka imani yako wapi juu ya kitu kingine chochote ila Neno? Kama Mungu alisema jambo hilo, shikilia kidole chako Kwake, Hiyo ni kweli. Halisogei. Inanyonya kutoka kwenye Kitabu cha Mungu chenye maziwa, Biblia, sifa Za—Zake, yale aliyoahidi. Yale aliyoahidi, hilo ni Neno Lake. Neno hujizaa Lenyewe. Linapaswa kuwa ni wazo kabla halijakuwa Neno, halafu Neno; ndipo Neno linadhihirishwa, na hapo ndipo unapotoa nguvu za—zako. Kuamini! Kuamini! Kwa ajili ya Muumba. . . Kuamini, kama vile alivyokuwa, Muumba aliyeumba ulimwengu.

¹⁷⁸ Agano Jipya lilisema, hapa nyuma, “Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa.” Kusudi lile lile. Ilikuwa ni kitu gani? Walikuwa wakimshuku Mungu, ndipo maradhi na shida zikaingia. Ndipo akamwinua yule nyoka. Kwa kusudi gani? Kwa ajili ya uponyaji wao na msamaha wao. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Na shaba inawakilisha hukumu ya Kiungu; naye Yesu alikuwa ndiye yule nyoka aliyehukumiwa, naam, neno shaba.

¹⁷⁹ Sasa, baada ya Yeye kuthibitisha lile Agano, ama agano lilipodhihirishwa kwake, inawapa imani watoto wa kweli wa Mungu. Neno huwapa imani, Mwenye Maziwa. Lina—linawafanyia jambo fulani wakati Ne—Neno, ama wakati agano linapodhihirishwa, linawapa imani wana wa kweli wa Mungu.

¹⁸⁰ Sasa tunajua, tunatambua ya kwamba, katika jambo hili, Yeye aliitwa Elohimu. Neno hilo pia, katika fasiri hapa, linamaanisha “Elohimu.” Nimeliangalia tu hivi karibuni, nipate kuwa na uhakika. Elohimu! Na *Elohimu* ni “Anayejitosheleza kwa Yote.” Yeye ni El Shaddai, Elohimu, Mungu Mwenye Maziwa, Anayejitosheleza kwa Yote. Hahitaji kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote. Yeye ndiye utoshelevu wako wote.

¹⁸¹ Angalia, jambo lilo hilo linashuhudiwa hapa, nilikuwa nikiangalia alasiri ya leo wakati nilipokuwa nikisoma, katika Ayubu, Ayubu. Yeye anaitwa “Elohimu.” Naye Ayubu alidhihakiwa, akafanyiwa mzaha; vipi, ni picha ya jinsi gani leo. Lakini Ayubu alikuwa akipumzika katika ahadi ya Elohimu, “Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo

katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mimi binafsi.” Akipumzika katika Elohimu, hata kitu gani kije.

¹⁸² Mkewe alikuja, akasema, “Unaonekana mnyonge sana, Ayubu.” Na hawa hapa wafariji wake wanakuja, “Loo, unaona yaliyokupata, mzee? Nilikwambia ulikosea, wakati wote. Unaona yaliyotukia?” Watu wengi wanapenda kuwalaumu watu kama hao.

¹⁸³ Ayubu alikuwa ndiye mtu mkamilifu sana katika siku yake. Mtu mkamilifu kuliko wote ambaye Mungu alikuwa naye duniani alikuwa ni Ayubu. Alimwambia Shetani, “Hapana mtu aliye kama yeye.” Amina. “Je! umemwangalia?”

¹⁸⁴ Shetani akasema, “Naam, anapata kila kitu kwa urahisi. Vunja wigo huo na uniruhusu nimpate. Nitamfanya akulaani mbele za uso Wako.” Alifanya kila aliloweza, bali hakufanikiwa.

Ayubu alitulia kwenye hiyo ahadi.

¹⁸⁵ Hao jamaa walimtembelea, na kusema, “Sasa, sasa yuko wapi Mungu huyo wako mkuu kabisa uliyekuwa ukinena habari Zake? A-ha, angalia vile ninii, u—unamwamini Yeye kuwa hivi, angalia—angalia yanayoendelea sasa.”

¹⁸⁶ Lakini bado alitulia kwa El Shaddai, hata haidhuru kama majipu yake yalikuwa yakimtoka na uhai wake ulikuwa karibu kwisha. Alikuwa ameketi juu ya lundo la majivu, akikuna majipu yake.

Mkewe akasema, “Wewe...Mbona usimkufuru Mungu upate kufa?”

Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu.” Loo, jamani!

¹⁸⁷ “Bwana alitoa, na Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe. Ninamtumaini Elohimu. Hata akiuangamiza mwili huu, mabuu ya ngozi yaule, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, ambaye nitamwona mimi binafsi; macho yangu yatamtazama wala si mwingine.” Alifufuka, katika Mathayo 27, wakati watakatifu walipofufuka, wakatoka kisha wakaingia, lakini ninii sana...wakaingia mjini. Ni mfano kamili wa siku hizi, tungali tukiingojea, tukitumainia ile ahadi.

¹⁸⁸ Angalia baada ya Yeye kutokea katika Jina hili, Jina la Mwenyezi Mungu.

¹⁸⁹ Sasa, kanisa, sasa tunaweza tukapata fundisho dogo hapa, huenda likawasokota kidogo. Kama hamliamini, hiyo ni juu yenu. Tuko tu hapa, nitazungumza tu yale ninayowazia. Una haki ya kuwazia yale unayotaka kuwazia.

¹⁹⁰ Lakini, angalia, bali mambo haya yote yalikuwa ni “vielelezo, vivuli, na mifano,” kama vile Biblia ilivyosema yalikuwa. Ndivyo yalivyo yote. Na hili nalo ndivyo lilivyo, Mungu anamshughulikia Ibrahimu safarini, kama tu

atakavyoushughulikia Uzao wa kifalme wa Ibrahimu safarini. Angalia, aliwashughulikia Wayahudi vivyo hivyo. Yote yalianzia kule, katika hiyo ahadi ya lile agano; mataifa yote, watu wote.

¹⁹¹ Angalia baada ya kutokea katika Jina hili la Mwenyezi Mungu. Na alifunuliwa ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Yule Anayejitosheleza kwa Yote. Hakuwa na wasaidizi; hakuhitaji wowote, makatibu wowote. Alikuwa peke yake, Mungu. Alikuwa ni Mungu, peke yake. Naye alimtokea Ibrahimu katika Jina hili, na wakati alipomtokea katika Jina hili, na Ibrahimu akatambua kwamba Yeye alikuwa ni Nani, alibadilisha jina la Ibrahimu. Sasa amefikia kwenye utimilifu wa kuamini sasa. Unaona mahali Kanisa limefikia? Ninatumaini mnaweza kusoma katikati ya mistari. Amefikia mahali ambapo Yeye amemfunulia kwamba Yeye alikuwa ni Nani, na ndipo akalibadilisha Jina la Ibrahimu ili kwamba ahadi ipate kutimizwa.

Sasa unasema, “Jina halina maana yoyote.”

¹⁹² Basi ni kwa nini alibadilisha jina la Ibrahimu kutoka Abramam likawa Ibrahimu? Kwa nini akabadilisha jina la Yakobo kutoka Yakobo, “mtwaa mahali pa mwingine,” likawa Israeli, “mtawala pamoja na Mungu”? Kwa nini akabadilisha Jina la Sauli likawa Paulo? Hakika, jina lake, hakika, hakika lina maana fulani. Hakika lina maana fulani. Kama hujapewa jina zuri, Mungu atalibadilisha, kama Yeye amekuita. Naam, bwana.

¹⁹³ Angalia, Yeye alibadilisha jina lake hapa sasa, kutoka Abramam likawa Ibrahimu, ambalo maana yake ni, “baba wa mataifa,” akaongeza h-i-m-u, Ibrahimu. Kwa hiyo alifanya jambo hili kusudi ahadi kamilifu ipate kutimizwa. Na mwana sasa, ambaye alikuwa ameahidiwa kwa muda mrefu, angeweza kuonekana, ama, vinginevyo, kufunuliwa, wakati Yeye alipobadilisha jina lake na baada ya kutambua Yeye alikuwa ni Nani. Huenda alikuwa, huenda alifikiri kwamba walikuwa ni kundi; bali alitambua ya kwamba Yeye alikuwa ni Elohimu, Mungu peke yake. Lakini, wakati alipofanya jambo hilo, basi alibadilisha jina lake. Akasema, “Sasa, Ibrahimu, wewe huitwi tena Abramam, bali Ibrahimu, kwa kuwa, ‘baba wa mataifa,’ nimekufanya.” Ibrahimu, sasa, yeye yuko katika hali nzuri sasa. Yuko katika hali nzuri baada ya ufunuo ya kwamba Yeye ni Nani. Sasa yeye yuko katika hali nzuri ya kuona mwana akifunuliwa.

¹⁹⁴ Mwana yuko tayari kuja, kufunuliwa. Loo, enyi watoto wa Ibrahimu!

¹⁹⁵ Angalia, Yeye alibadilisha jina la mjumbe Wake, moja kwa moja katika wakati wa mwisho. Kwa ninii tu, alikuwa na tisini na tisa, umesalia mwaka mmoja, ndipo akabadilisha jina lake kutoka Abramam likawa Ibrahimu. Kwa kubadilisha jina lake, akaongezea h-i-m-u, ambalo maana yake ni “baba.” Yeye alikuwa awe baba, baba wa ahadi; baba, ahadi.

¹⁹⁶ Loo, kama una utambuzi wa kiroho, sikiliza! Baada ya ufunuo wa Jina Lake, kwamba Yeye alikuwa ni Nani, Yeye alimbadilisha jina lake. Sasa baada ya ufunuo, sasa Yeye alishuka duniani, “hakuna kundi la Miungu; kuna Mmoja,” sasa wakati umewadia wa ufunuo wa Mwana ambaye ameahidiwa kufunuliwa kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, wa ile ahadi.

¹⁹⁷ Tazama, Yeye alilibadilisha kutoka Wesley, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste. Sijui kama niseme jambo hili au nisiliseme. Haikulazimu kuliadini. Lakini ninatumaini mtanisamehe, kwa maana sitaki kuwaudhi.

¹⁹⁸ Lakini, tazameni, hapajapata kuwa na mjumbe kwa makanisa ya—ya Mungu, kote katika historia yote ya wakati, ambapo walipata kuwa na kiongozi, tangu yale matengenezo, kama kiongozi tuliye naye leo, Billy Graham, naam, maana ameenda kote ulimwenguni. Unaona? Pia, tazameni, kamwe hatujapata kuwa na mtu, mtengenezaji yeyote. . . Tunamchukua Sankey, Moody, Finney, Calvin, Knox, yeyote yule, Wesley, Luther, hakujakuwako na mmoja mwenye jina linaloishia katika h-a-m, siku za nyuma. Mjumbe pekee tuliyepata kuwa naye katika nyakati za kanisa, akiwa na jina linaloishia na h-a-m; G-r-a-h-a-m, Graham.

¹⁹⁹ Na Graham ni herufi sita, na sita ni namba ya binadamu, siku ya binadamu; mtu aliumbwa, katika—katika Mwanzo 1:26, katika siku ya sita. Lakini saba ni namba ya Mungu; siku ya saba, Mungu alipumzika. Si sita, ikionyesha huyu G-r-a-h-a-m angekuwa ni kwa kanisa ambalo liko ulimwenguni; lakini, A-b-r-a-h-a-m, Abraham ni herufi saba.

²⁰⁰ Unasema, “Namba hazina maana yoyote.” Basi wewe hujui tarakimu za Biblia yako. Unaona? Huna budi kukosea sasa. Bila shaka.

²⁰¹ Mungu “hukamilishwa” katika *tatu*, na “kuabudiwa” katika *saba*, na “kujaribiwa” katika *arobaini*, na “yubile” katika *hamsini*, loo, chochote unachotaka kufanya. Hesabu zote, Biblia huenda kwa hisabati.

²⁰² Tazama, wa sita ni mjumbe atakayetumwa kwa ulimwengu. Na, angalia, saba ni nambari ya Mungu.

²⁰³ Basi angalia katika wakati huu wa kutokea sasa, ama kufunuliwa kwa Mwana. Wakati ninii. . . Atakapofunuliwa, Mwana. Tayari wamelitambua Jina Lake, wamejua Yeye alikuwa ni Nani. Yeye ni El Shaddai, Mwenyezi, Elohimu. Lakini sasa tunafikia wakati ambapo Mwana aliyeahidiwa atajifunua. Mwana, Isaka Mwenyewe ambaye ameahidiwa, yuko tayari kujitokeza jukwaani.

²⁰⁴ Wala asingeweza kufanya jambo hilo mpaka alipotuma na kubadilisha jina lake kutoka Abramum likawa Ibrahimu, kwa maana, “yeye alikuwa, baba wa mataifa.” Angalia, *-himu*. h-i-m-u “baba, baba wa mataifa.”

²⁰⁵ Angalia jinsi hilo linavyoafikiana na Malaki 4, “Kuirejesha Imani, iwarudie baba zao,” Uzao wa Ibrahimu urejeshwe kwenye aina ile ya Imani ambayo baba Ibrahimu alikuwa nayo, Uzao Wake wa kifalme. Malaki 4 kutimizwa, ni kurudisha Imani iliyokuwa huko nyuma mwanzoni, kuirejesha kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Ni ahadi. Ni ahadi kabisa. Uzao wa Kifalme utafunuliwa, na kwa ninii. . . kwa Uzao wa Kifalme, ambao ni Uzao wa Kifalme, wa Kristo. Kristo ndiye Uzao wa Kifalme. Na huo Uzao ni Roho Mtakatifu aliye ndani ya mioyo ya watu wanaomwamini Mungu, wanalishikilia Neno Lake, na Mungu akitenda kazi kupitia kwao, akiendeleza Ujumbe ule ule. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, hata hivyo mtaniona; nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Na kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaona, akifunua hayo katika siku za mwisho hapa, jinsi inavyopaswa kuja.

²⁰⁶ Sasa, angalia mlango wa 18 sasa. Mara baada ya jina lililobadilishwa, Mungu anatokea, apate kujifunua Mwenyewe katika mwili. Baada ya jina kujulikana, kwamba Yeye ni Nani, Mungu anajitokeza katika mwili. Ibrahimu, siku moja yenye joto, majuma machache tu ama miezi kabla Sodoma haijateketezwa na Isaka kujitokeza jukwaani. Na, angalieni, Ibrahimu ameketi nje chini ya mwaloni wake.

²⁰⁷ Naye Lutu yuko huko chini Sodoma, nao wanafurahia anasa za ulimwengu. Hata hivyo, yeye ni Mchungaji Lutu, labda alikuwa amejipatia maskini kusanyiko dogo zuri huko chini. Lolote alilofanya, Biblia ilisema, “Uovu na dhambi za— za wakati huo ziliitesa nafsi yake yenye haki.” Kwa hiyo hapana budi alikuwa ni kama Lutu wengi wa siku hizi leo, bali alijua asingeweza kusema lolote juu ya jambo hilo. Kwa hiyo basi angalia, akawa ndiye huyo hapo.

²⁰⁸ Lakini Ibrahimu, alipokwisha kufunuliwa kwake, sasa, Elohimu ndiye aliyekuwa akisema naye. Sasa yeye ameketi chini ya mwaloni, na hawa hapa watu watatu wanakuja, wakitembea kama wanadamu. Angalia matokeo ya ufunuo, ya kwamba Mungu alikuwa ni Nani, juu ya Ibrahimu, kile ulichomfanyia. Baada ya jina lake kubadilishwa kutoka Abramum likawa Ibrahimu, yeye aliwaona Watu watatu wakija, naye akawaita hao watatu, Mmoja, “Bwana wangu.” Watatu wao, wakiwa ni Mmoja. Sivyo ilivyokuwa na namba sita, Lutu; yeye aliwaona wawili wakija, naye akasema, “bwana zangu.” Ono na ufunuo wa Ibrahimu ulimwonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Elohimu Anayejitosheleza kwa Yote. Uzao wake utapokea jambo lile lile.

²⁰⁹ Angalia jinsi alivyojifunua Mwenyewe, jinsi alivyojitambulisha, kama alikuwa anasema kweli ama la. Angalia, kwa mwaminio wa kweli, ile ishara aliyofanya. Alifanyaje, kumfanya ajue ya kwamba huyo alikuwa ni Elohimu?

210 Sasa, yeye alisema, “Bwana wangu.” Ni herufi kubwa B-w-a-n-a. Msomi yeyote, unajua hivyo; msomi yeyote anajua huyo ni Elohimu, Anayejitosheleza kwa Yote, Elohimu.

Mtu mmoja aliniambia, wakati mmoja, “Huamini huyo alikuwa ni Mungu ati?”

211 Nikasema, “Hakika ninaamini. Ibrahimu alisema alikuwa ni Mungu. Alizungumza Naye; anapaswa kujua.” Naam.

212 “Loo,” alisema, “unamaanisha Mungu akisimama pale akila nyama ya yule ndama, na—na kunywa maziwa toka kwa ng’ombe, na akila ugali, chochote unachotaka kukiita pale?”

213 Nilisema, “Alikula. Kumbe, ni kwamba humjui Mungu wetu.” Vema, jamani, Yeye angeninii tu...Mbona, Yeye ananyosha tu mkono...

214 Tumeumbwa kwa elementi kumi na sita; petroli, nurulimwengu, na potashi, na kalisi, na kadhalika, elementi kumi na sita tu. Yeye alizichukua zote kwa pamoja, na kuzipulizia, na akashuka akatembea duniani. Nina furaha sana kwamba Yeye ni Baba wa aina hiyo. Ingawa mabuu ya ngozi yatauangamiza mwili huu, hata hivyo Yeye atakuita. Aliahidi atafanya hivyo. Yeye ni Elohimu. Akanyakua konzi nyingine, na kusema, “Njoo hapa, Pakanga,” ama yeyote yule, hao Malaika, “na tushuke chini. Hebu tushuke twende tukaangalie Sodoma, tuone ni kitu gani kinachoendelea.”

215 Ndipo Ibrahimu, baada ya huo ufunuo, aliona jambo hilo na akajua ya kwamba kulikuwa na Mungu mmoja. Naye aliona jambo hilo, na kusema, “Bwana wangu, njoo huku, keti, hebu nioshe miguu Yako.” Sasa, yeye kamwe hakusema, “bwana...” Na, angalia, liko katika—liko katika herufi kubwa pale. Mtu yeyote anajua hilo. Nina Kamusi Fafanuzi. Mnaona, ni herufi kubwa B-w-a-n-a, “Bwana,” Elohimu, Anayejitosheleza kwa Yote. Kasema, “Hebu nilete maji kidogo nioshe miguu Yako, na nikupe kipande kidogo cha mkate, ndipo unaweza kwenda Zako.”

216 Aisee, ninachelewa sana hapa. Afadhali niharakishe. Ni—ninataka kufikia hapa, wala sijui ni wakati gani nitakapoweza kupafikia. Nivumilieni tu muda kidogo zaidi, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

217 Angalia, Elohimu, Anayejitosheleza kwa Yote, Mungu. Naye akasema...Angalia aliyofanya.

218 Sasa, wawili Wao walianza, walikaza ku—kuangalia huko Sodoma.

219 Naye akasema, “Je! mnafikiri nitamficha Ibrahimu siri hii?” Yeye hafanyi lolote mpaka amelifunua kwa manabii Wake. Unaona, Yeye huwajulisha jambo hilo. Ndipo akasema, “Sitamficha jambo hili, kwa kuwa yeye—yeye amebarikiwa na Mungu naye atairithi nchi, na kadhalika. Uzao wake utairithi,

vinginevyo, atakuwa baba wa mataifa mengi. Sitamficha. Nitamjulisha.” Na kwa hiyo akasema, akaanza kumfunulia.

²²⁰ Ndipo akasema, “Ibrahimu,” si Abram. “Ibrahimu, yu wapi S-a-r-a, mkeo?” Yeye alijua jamba hilo? Vema, siku moja tu kabla ya hapo, yeye alikuwa Abram, siku moja au mbili kabla ya hapo. Naye alikuwa Sarai, na sasa yeye ni Sara. Naye ni Ibrahimu. Kasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Ibrahimu akasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.”

²²¹ Akasema, “Nitakurudia wakati huu huu mwakani. Na mwana huyu ambaye ameahidiwa, yuko tayari kuja jukwaani sasa. Utampata.”

²²² Naye Sara, kwa nafsi yake, kwa namna fulani akacheka, kasema, “Niwapo mkongwe, ati nipate raha na bwana wangu tena, naye ni mzee?” Kitu kama hicho, kwa hiyo, maana yeye alikuwa—alikuwa na tisini, naye alikuwa na mia moja. “Na kwa hiyo sasa ningeweza kufanya jambo hilo tena?”

²²³ Naye Malaika huyo, mjumbe, Mungu katika mwili wa kibinadamu, akasema, “Mbona yeye amecheka?”

²²⁴ Hilo lilikuwa ni thibitisho. Kwa nini? Ilionyesha ule ufunuo ulikuwa wa kweli. Ilionyesha kwamba vile alivyokuwa amemwita Yeye, Elohimu, ilikuwa ni sahihi. Kwa sababu, Yeye alikuwa ni Neno. Hiyo ilikuwa ni ninii... Katika Waebrania, mlango wa 4, kifungu cha 12, ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Na wakati Ibrahimu alipoona jambo hili, alikuwa na hakika basi angeweza kumwita, “Elohimu.” Elohimu, Yeye alikuwa Neno, “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²²⁵ Angalia wakati Yesu, Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, alipojitokeza jukwaani, Yeye alijifunua Mwenyewe kwa uzao wa kawaida wa Ibrahimu, katika ishara ile ile. Nao wakamwita, “Beelzebuli.” Iliwapofusha, hao wasioamini, iliwapofusha na kuwafanya wakufuru, na kuwapeleka kuzimu. Lakini iliwapa waaminio mwangaza wa Milele, hao waliokusudiwa uzima wa Milele.

²²⁶ Angalia, Yesu aliahidi ya kwamba ninii...katika siku za mwisho, kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu, ya kwamba angekuja na kujifunua Mwenyewe, katika siku ambapo Mwana wa Adamu anafunuliwa, Uzao huu wa kifalme wa Ibrahimu ungeona ishara ile ile. Sasa angalia, wakati Yeye aliposema, hiyo—hiyo ni Luka Mtakatifu 17:28 na 30, “Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Sasa, Yesu alisema jambo hili. Mimi siwajibiki kwalo. Yeye... Ninawajibika katika kulisema, kusema kile alichosema. Lakini, Yesu alisema hivi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kule kuja, katika kuja Kwake Mwana wa Adamu,”

sasa angalia, “katika siku atakayofunuliwa Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa kwa Kanisa Lake.”

227 Kama vile kwa Ibrahimu. Yeye alikuwa Mungu, aliendelea kushuka chini, akathibitisha lile agano, akatambua Yeye alikuwa ni Nani, na jina lale likabadilishwa. Angalia, lilibadilika kabla tu hajafika juu ya kilima, akiangalia Sodoma, kabla tu ya kuja kwa yule mwana aliyeahidiwa.

228 Yesu alisema picha ile ile. Yesu alikuwa akisoma Biblia ile ile ninayosoma na unayosoma wewe. Kama ukitaka kujua ilikuwa ni ipi, rudi nyuma uone yale waliyokuwa wakifanya katika siku za Sodoma. Angalia, si sana katika siku za Nuhu (Alinena juu ya utovu wao wa uadilifu, jinsi walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa), lakini katika Sodoma.

229 Sasa “hakuna maji tena,” Mungu aliahidi jambo hilo kwa ishara ya upinde wa mvua. Yeye alitupa ishara. Yeye daima hutoa ishara. Upinde wa mvua. . . Yeye daima hukumbuka ishara Zake. Daima ni mwaminifu kwazo miaka yote, kamwe hakosi kutoa hiyo ishara ya upinde wa mvua. Yeye daima hutoa ishara Zake. Angalia.

230 Na katika ishara hiyo, Yeye aliahidi kutouangamiza ulimwengu “kwa maji tena,” bali alisema “ungeungua moto.” Na angalia Yesu hapa akisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” ulimwengu wa Kimataifa ulikuwa unaenda kuangamizwa. Walawiti!

231 Sasa angalia huo uadilifu wa mataifa. Angalia utovu wa uadilifu wa kanisa, ni kama tu Lutu. Angalia ni kitu gani kilicho kule chini miongoni mwao: mtu fulani, G-r-a-h-a-m, akiwakemea vikali, hao wanasiasa, kwa hilo kanisa la kawaida. Sasa katika kanisa la kiroho. . .

232 Daima kuna matabaka matatu ya watu. Hayo ni, waaminio, wasioamini, na wanaojifanya waaminio. Wanao katika kila kundi la watu. Kama mngehisi msukumo niliosikia, mngejua walikuwa papa hapa usiku wa leo. Kwa hiyo, basi, ninyi. . . na yote matatu. Angalia, haya basi, daima kuna hayo matabaka matatu ya watu kila mahali.

233 Sasa kama utaona ya kwamba ilikuwa iwe ni jambo lile lile wakati Mwana wa Adamu alikuwa afunuliwe kwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, kupitia kwa Kristo (Kristo ndiye Uzao wa Kifalme), wakati anapofunuliwa katika siku za mwisho. Sasa, mahali ulipo, ulimwengu uko vivyo hivyo, kwa maana Mwana aliyechomoza Mashariki anatua Magharibi. “Na ilikuwa ni siku ya utusitusi,” waliunda mashirika, madhehebu, “lakini itakuwa Nuru wakati wa jioni,” alisema nabii Yereimia. Sasa, na katika siku ambazo Mwana huyo, atakapotokea nyuma ya mawingu ya madhehebu, kujifunua Mwenyewe, Yeye alisema ulimwengu ungekuwa kama tu ulivyokuwa katika siku za Sodoma, na Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe tena kwa watu Wake.

Angalia jinsi Yeye alivyolifunua kwa uzao wa Isaka; angalia jinsi Yeye atalifunua kwa Uzao wa kifalme, Bibi-arusi wa Kifalme, yule Malkia. Malkia ni Uzao wa kifalme.

²³⁴ Kama vile Mungu alivyotoa taifa kutoka katika taifa, kule Misri, Yeye analitoa Kanisa kutoka katika kanisa, ama Bibi-arusi kutoka katika kanisa; Kanisa kutoka katika kanisa. Na Uzao wa mwanamke uliosalia, hao ni wale waliosalia, “kuna kulia na kuomboleza na kusaga meno, maana hawakuwa na Mafuta katika taa zao, Roho Mtakatifu,” daima aliwakilishwa. Hao hapo.

²³⁵ Hali ya mambo iko sawa. Na sasa angalia huko juu ya kilima. Sasa, Kanisa, Ibrahimu; Lutu; Wasodoma. Ulimwengu; kanisa; Wateule. Kanisa, Bibi-arusi, nje ya kanisa. Tumeketi vizuri mahali petu. Ulimwengu uko katika mdundo halisi kwa jambo hilo.

²³⁶ Upotovu! Kila kitu kimepotoshwa. Hiyo ni kusema, nitawaambia, kila kitu ni zaotuka. Wao . . .

²³⁷ Nilishuka nikaja, nikaona ishara kubwa, ilisema, “Mahindi zaotuka.” Kumbe, hayafai kitu. La. Hilo linapaswa kuwafanya ninyi makafiri kuruka. Wakati Mungu aliposema, “Kila mbegu na izea kwa jinsi yake.” Nanyi mnaweza kuyazalisha mahindi na kuyafanya yaonekane bora, bali hamwezi kuyapanda tena; hayana uhai ndani yake.

²³⁸ Na hivyo ndivyo tumelifanya kanisa. Tumelirembesha, na kulipamba vizuri kwa zari za kimadhehebu, bali halina Uhai ndani yake. Haliwezi kutoa ushuhuda huo wa Biblia tena. Mnaona? Haliwezi kutoa ushuhuda wa kufufuka kwa Kristo. Ni mambo ya zaotuka.

²³⁹ Watu waliovalia vizuri zaidi, wanalipwa vizuri zaidi, madhehebu makubwa zaidi, matajiri zaidi, wa Wakati wa Laodikia, kweli kabisa. “Tajiri, sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, mwenye mashaka, kipofu, na maskini, uchi, nawe hujui.” Kama mtu alijua alikuwa uchi, ungeweza kuzungumza naye. Lakini wakati yeye hajui hilo, hiyo ni hali ya mashaka, ya kusikitikisha. Usiwadharau watu hao, bali wahurumie. Vipi kama huyo angekuwa ni wewe katika hali hiyo? Vipi kama Neno halikufunuliwa kwako, ungefanya nini? Ni kitu gani tena kingejalisha, kama macho yako yalikuwa mapofu sana usingeweza kuona Hilo? Hiyo ni hali ya mashaka.

²⁴⁰ Na vivyo hivyo tu, kwenye hali hiyo. Huwezi kulielekezea kidole; hilo hapo limekaa, jinsi hasa Yeye alivyosema ingetukia. “Ishara hizi zitakuwako katika siku za mwisho.” Angalia mahali zilipo, vivyo hivyo kabisa.

²⁴¹ Sasa angalia, kuchanganya mbegu. Mwajua, kama chochote mimi . . . Hebu chukua, kama vile ungechukua pu—pu—pu—punda, na umzalishe kwa farasi, farasi jike, hasa, nawe unapata kitu gani? Unapata nyumbu. Lakini huyo nyumbu hawezi

kuzaa tena. Unaona? Mungu alisema, “Kila mbegu na izea kwa jinsi yake.” Sasa ivolusheni yako inatokea wapi? Mradi wako mwenyewe umekataa kile ulichosema unaamini. Mungu alisema, “Kila mbegu na izea kwa jinsi yake.” Hawezi kuzaa kamwe. La, la. Amekwisha.

²⁴² Pia nafikiri nyumbu ni mmoja wa vitu vijinga mno nilivyopata kuona. Huwezi kumfundisha chochote. Ataketi hapo na hayo masikio makubwa marefu, unajua, naye atangojea mpaka dakika ya kufa hasa akupige teke, kabla hajafa. Yeye ananinii tu. . .

²⁴³ Huwezi kumfundisha chochote. Inanikumbusha. . . Ataketi hapo, nawe utanza kumwambia mambo, inanikumbusha juu ya watu fulani, wanaodai ni waaminio leo. Masikio makubwa marefu, wanaketi pale, na, “Siku za miujiza zimepita. Hoo! Hoo! Hoo!” Hajui anakotoka. Hajui lolote kuhusu jambo Hilo. Jambo pekee ajualo ni baadhi ya kanuni za imani za kanisa.

²⁴⁴ Lakini hebu niwaambie, ninaheshimu asili bora. Jamani, anaweza kukwambia ukoo wake. Anaweza kukwambia baba yake alikuwa nani, mama yake alikuwa nani, bibi yake alikuwa nani, babu yake alikuwa nani. Yeye ni asili bora.

²⁴⁵ Ndivyo walivyo hao Wakristo wa asili bora, wanaweza kurejea moja kwa moja kwenye Kitabu cha Matendo na kuona mahali walikotoka, Mkristo wa asili bora, aliyezaliwa kwa Roho yule yule, jambo lile lile, akitenda vile vile.

²⁴⁶ Pamoja na watesaji wale wale; punda na farasi wakila pamoja. Hiyo ni kweli. Haya basi. Huna budi kuwa na jambo hilo, hata hivyo. Hii ni siku ya zaotuka.

²⁴⁷ Niliona makala kwenye *Reader's Digest*, si muda mrefu uliopita, “Mkiendelea kuwalisha wanawake nyama hii ya zaotuka na—na takataka hizi, hawawezi kupata watoto wao. Wamebadilika. Wanakuwa wapana mabegani, na wembamba kiunoni.” Kwa nini, ni, unajua mwanadamu daima hujiangamiza mwenyewe kwa ustaarabu.

²⁴⁸ Mrudieni Mungu! Mwaminini Mungu. Rudini kwenye Mbegu ya asili. Rudini mwiamini. Mmesoma ka. . . mna kanda zangu, hasa, nadhani mlizisikia, juu ya: *Mbegu ya Asili*, na *Mti wa Bibi-Arusi*, na mambo hayo, ambayo ni kweli. Bwana anajua jambo hilo.

²⁴⁹ Jinsi mambo hayo yametabiriwa, miezi na miezi. Ninyi watu, mnachoona hapa, ni kidogo tu, mnayoona yakitukia. Waulizeni watu wa siku nyingi, waulizeni kama kuna wakati mmoja imeshakosea. Inasema mambo ya watu, matetemeko ya nchi, mambo yatakayotukia. Roho Mtakatifu anatwambia. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Kuna mtu ambaye amekuwa. . . Hakika. Na kuhusu watu mbalimbali.

²⁵⁰ Ni kama vile Marilyn Monroe, muda mrefu sana kabla hajakufa. Wao walisema ya kwamba alijinyonga. Hakujinyonga. Alikufa kwa ugonjwa wa moyo. Kweli kabisa.

²⁵¹ Mtu huyu, mpiganaji huyu. Ile Ngome ya Maginot huko Ujerumani. Mambo hayo yote, maelfu tu ya mambo, juu ya alama barabara, kila wakati. Haiwezi kuwa ni kitu kingine ila ni Roho Mtakatifu. Mnaona? Mnaona? Yeye aliahidi jambo hilo.

²⁵² Yeye alitangaza mambo saba katika mwaka wa 1933, yangetukia. Na sasa kila moja ya hayo limetukia ila mambo mawili, kikamilifu, kabisa juu ya alama. Jinsi vile ambavyo hata Rais Kennedy angechaguliwa. Yako pale pale kwenye vitabu vyangu sasa hivi, yalisemwa miaka thelathini na mitatu iliyoipita, sawasawa kabisa. Jinsi ambavyo ile Ngome ya Maginot ingejengwa, miaka kumi na mmoja kabla haijajengwa. Jinsi ambavyo Hitler angeibuka, na—na Ufashisti, na—na Unazi, na hizo zote kuishia katika ukomunisti, nao ukomunisti ungeungamiza Ukatoliki. Na utauangamiza, naam, haidhuru wafanye nini. Na akaonyesha, akasema kungekuwa na Baraza la Ekumeni, na jinsi ambavyo makanisa yote yangeungana pamoja na yangefanya sanamu inayoitwa Alama ya Mnyama. Unayaona moja kwa moja yako njiani, sasa hivi. Kweli kabisa. Halina budi kutukia, maana hakijashindwa kamwe.

²⁵³ Mtu yeyote ambaye amepata kujua jambo hilo, mtu yeyote, wachukue kote ulimwenguni, hakijakosea kamwe hata wakati mmoja. Miezi na miaka kabla ya wakati wake, ni kamilifu kabisa juu ya alama. Ni Mungu miongoni mwenu, enyi watu; Mungu ndani yetu, Roho Mtakatifu. Angalia, Yesu alisema ya kwamba Uzao wa kifalme ungetambulishwa na jambo lile lile, hapa katika Luka mlango wa 17. “Loo, rudini, Enyi mliotawanyika, kutoka katika madhehebu yenu, rudini makwenu.”

²⁵⁴ Yeyote wetu anaweza kumwamini Mungu huyo... Kama unamwamini Mungu, unajua Mungu huwaponya wagonjwa. Hilo si swali. Mbona, kama huamini jambo hilo... Unajua, walisema katika siku hizo, “Yehova, tunajua anaweza kuponya, bali hawezi kuokoa.” Sasa, “Yeye anaweza kuokoa, bali hawezi kuponya.” Unaona, ibilisi yule yule tu, jambo lile lile. Yeye ni Mwokozi na mponyaji pia. Yeye ni Yehova-Yire na Yehova-Rafa.

²⁵⁵ Loo, rudini! Kumbukeni, Yeye aliahidi mahali tulipo, kuhusu kila kitu kikiwa jinsi tu kilivyo sasa, yale ambayo yangetukia. Alisema yangetukia, na hayana budi kutukia.

²⁵⁶ Jamani, nasikitika. Nimewachelewesha sasa. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, nitaninii... Nitamalizia hili, labda, kesho usiku. Nina kama kurasa nyingine sita hivi za mihitasari hapa. Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja. Iweni na kicho, kila mtu.

²⁵⁷ Huenda msikubaliane nami; mna haki ya kufanya hivyo. Nina haki ya kusema ninayowazia. Nimekuwa na Maandiko

hayo. Sasa, haidhuru ningesema nini, kama Mungu haungi hayo mkono, basi Urimu Thumimu haifanyi kazi, basi imekataliwa. Haidhuru linasikika ni zuri jinsi gani na linasikika ni halisi jinsi gani, Urimu Thumimu haina budi kulionyesha. Mbegu haina budi kuchipuka. Kama haichipuki, basi haikuwa kweli.

²⁵⁸ Sasa, kwa ajili ya uponyaji, nimejaribu kuwaambia ya kwamba mimi si mponyaji. Kuna watu wengi wanaojiita waponyaji. Halafu kuna wananii wengi—kuna wakosoaji wengi sana wanaowaita watu waponyaji, ili kwamba, wapate kukosoatu. Moyo wao haupatani na Mungu. Unaona? Mtu yeyote anajua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kumponya mwingine. Mungu huponya magonjwa. Hebu Mungu aagize kifo chako, na uombe yote utakayo, na hospitali ikudunge sindano ya giligili kila siku, nawe utakufa haidhuru.

²⁵⁹ Kama nikiukata mkono wangu usiku wa leo, na nisimame hapa na mkono uliokatwa, hakuna dawa ulimwenguni inayoweza kuuponya mkono wangu. Hatuna dawa inayoponya. Hakuna dawa inayoponya. Daktari yeyote atakwambia hilo. Inauweka safi tu wakati Mungu akiponya. Haiwezi kujenga tishu. Kama nikiukata mkono wangu, na, “Loo,” mnasema, “naam, Ndugu Branham, kuna dawa inayoponya huo.” Vema, ninataka kujua ni dawa ipi.

²⁶⁰ Hebu niwaonyeshe. Kama nikiukata mkono wangu na nianguke hapa chini nife, daktari angeweza kuja na kuutia mwili wangu dawa usioze na kunifanya nionekane kawaida kwa muda wa miaka hamsini. Aushone mkono wangu, na anipeleke huko nje na kunidunga sindano ya penisilini, kila siku, na miaka hamsini kutoka sasa jeraha hilo litakuwa kama tu lilivyokuwa wakati lilipotiwa. Kama—kama dawa zilitengenezwa zipate kuponya jeraha, kwa nini zisiliponye? Dawa yoyote itakayoponya jeraha mkononi mwangu, itaponya jeraha kwenye dawati hili, ingeponya jeraha kwenye koti langu. Kama ingeponya jeraha, itaponya jeraha haidhuru liko wapi. “Vema,” unasema, “mbona, dawa zilifanywa kwa ajili ya wanadamu.” Basi kwa nini haiponyi? “Vema,” unasema, “uhai umekutoka.” Basi kuna kitu kingine mbali na dawa kinachoponya.

²⁶¹ Ni uhai, hakika, na uhai ni Mungu. Hakika, ndivyo ulivyo. Hata hivyo, wengine ni wenye dhambi, wamepotoshwa nayo, bali hata hivyo wewe uko katika mfano wa Mungu. Na uhai ulio nao huo ulipewa na Mungu. Unajua hilo; la, kwa sababu Mungu ndiye mponya. Uhai ndio mponya. Mnaamini hilo, unaona. Mmeona mengi sana yakifanywa.

²⁶² Sasa hebu na tumkubali tu, sivyo? Kabla hatujafanya jambo hilo, sijui ni wangapi humu ndani wameshawishika, kabla... Kama ninyi ni wageni hapa, hamjawahi kuja hapa siku za nyuma, kwamba mnamwamini Yeye kwamba ni Mwana wa

Mungu? Na kwa jambo hili, Ujumbe huu usiku wa leo, Neno peke yake, kabla hata hajafanya jambo lolote, ya kwamba unaliadini, na unataka nikukumbuke katika maombi, inua mkono wako. Utafanya hivyo? Loo! Mungu awabariki. Loo, jamani! Mikono mia tatu ama mia nne. Mungu awabariki.

²⁶³ “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Sababu ya mimi kusema jambo hilo, Uzao utapata kibali kwa Mungu. Nafikiri sasa, badala ya—ya kuita tu mstari wa maombi hapa juu, nitawaacha tu ninyi muombe.

²⁶⁴ Hebu niwape Maandiko, kwanza. Tunayofanya, hayana budi kuwa ya Kimaandiko. Hayana budi kuwa ya Kimaandiko! Mungu hata kubali kitu kingine. Mungu hatathamini uongo; mnajua jambo hilo. U—usingeweza kumbandika huo. Yeye hathamini uongo. Yeye huthamini tu Neno Lake. Lakini aliahidi, ya kwamba, “Neno Langu halitanirudia bure. Litatimiza yale lililokusudiwa.” Nasi tunaona Neno lililotengwa kwa ajili ya siku hii. Haidhuru kutokuamini kutainuka kambini jinsi gani, Mungu atalithamini Neno Lake wakati atakapopata hiyo imani ya kulithamini.

²⁶⁵ Sasa mahali fulani humu jengoni, ninataka mchukue Maandiko haya. Waebrania mlango wa 3, ninaamini ndipo. Biblia ilisema, ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.”

²⁶⁶ Nawe uliyeinua mkono wako, ninakutaka, mara ibada inapofikia mwisho wake hapa, nakutaka uje na kusimama hapa ukaombe, ukamkubali Kristo kama Mwokozi wako. Nenda zako kwenye moja ya kanisa zuri mahali hapa. Haidhuru liko wapi, mtu fulani anayehubiri Injili, waendee na uombe ubatizo wa Kikristo. Naye mchungaji atakuchukua kutoka hapo na kuendelea. Yeye ni mtu wa Mungu. Ameitwa apate kuwa mtu wa Mungu, ata—atakuchukua kutoka hapo na kuendelea. Ninii tu, kama ningekuwa nipo hapa kwenye jiji hili, ningekuwa mfuasi wa baadhi ya makanisa haya hapa. Ningeyajia, hayo yanayoamini Injili. Ningekuwa huko. Hakika, ningejitambulisha pamoja nayo, kwa kuwa hilo ndilo unalopaswa kufanya. Na hilo ndilo unalohitajika kufanya.

²⁶⁷ Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu, sasa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa hiyo ingembidi kufanya vile vile kama alivyofanya jana.

²⁶⁸ Sasa angalieni, maskini mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, wakati mmoja, Naye akageuka na kujua alikuwa na nini, na kumwambia imani yake ilikuwa imemwoko. Naye akahisi, ndani yake; hakujiambua kuthibitisha hilo. Haikumbidi kulithibitisha.

²⁶⁹ Huthibitishi mambo. Unamwamini Mungu. Unaona? Humthibitishi Mungu, hata kidogo. Huwezi kuthibitisha,

kuyaokoa maisha yako, kuna Mungu, kutoka nje hapa tu na kusema, “Hebu nimwone.” Unaona, inakupasa kumwamini.

²⁷⁰ Silaha zote za Mungu ni za kimbinguni. Upendo, furaha, imani, uvumilivu, subira, upole, unaona, zote ni za kimbinguni. Tunaviangalia vitu ambavyo huwezi kuviona kwa jicho lako la kawaida.

²⁷¹ Naye Kristo yupo hapa usiku wa leo. Yeye aliahidi jambo hilo. “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nipo hapo kati yao. Nipo hapo!” Huyu “Mimi” tena, Yeye yupo hapa. Sasa, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²⁷² Ninyi ombeni, na kusema, “Bwana Yesu, mimi ni mgonjwa,” ama chochote unachohitaji. “Ni—ni mhitaji, na ni—ninakuhitaji, Mungu mpenzi, unirehemu, na uniponye na unifanye mzima. Na sasa kama nina imani ya kutosha, Bwana, kukugusa Wewe. . . Ni—ninajua ya kwamba Ndugu Branham hanijui. Mimi ni mgeni. Nami ninajua hanijui. Sasa, kama—kama mtu huyo ameniambia Kweli, ambayo ninaamini ndiyo, maana inakuja moja kwa moja kutoka kwenye Neno Lako. Nimelisoma, nimeona linaonekana ni la kweli kabisa. Sasa lithibitishe. Ninadai kuwa mimi ni Uzao wa Ibrahimu, kwa njia ya Kristo, ninadai kuwa Uzao wa kifalme, nikimwamini Yesu Kristo, Uzao wa Kifalme. Nami ninaamini kuwa ni sehemu ya Bibi-arusi Wake, Kanisa Lake analolijia. Nami ni mgonjwa na ni mhitaji. Tafadhali, Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako. Na kuthi-. . . na unithibitishie kwa kunena kupitia Ndugu Branham, kama vile alivyoahidi ingekuwa ‘kama vile ilivyokuwa katika siku za Sodoma.’ Nijalie tu. . . jalia aniambie yale ninayowazia, ninayoomba, yale ninayotaka, haja zangu ni nini, kitu fulani kunihusu mimi.” Wewe fanya hivyo, hebu fanya hivyo tu.

²⁷³ Baba wa Mbinguni, sasa yote yako mikononi Mwako. Sasa haya tu ndiyo ninayoweza kufanya, ama mtu yeyote yule, anaweza tu kusema yale Wewe umekwisha kusema *Hapa*, ile Kweli. Sasa lithibitishe, Bwana, kuwa ni Kweli. Nimezungumza habari Zako. Nena kwamba nimesema Kweli. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁷⁴ Ninawatakeni ninyi kuninii tu—kuamini tu, iweni tu na imani. Sasa hebu mtu yeyote asitembeetembe. Ketini tu kwa uchaji sana. Ninawatakeni muwazie akisimama mbele zenu, hapa mahali fulani, Kristo, aliyefufuka katika wafu; alikuja akapitia kwenye kuta wakati mmoja, akala mkate, kasema, “Niguseni, Mimi ni nyama na mifupa,” kisha akatoweka moja kwa moja mbele zao. Sasa Yeye—Yeye aliahidi ya kwamba angetokea katika siku za mwisho, katika umbo la mwili wa mwanadamu tena, katika miili yenu, kama alivyofanya katika siku za Sodoma. Mungu, ambaye alikuwa ni Kristo, aliyedhihirishwa katika mwili, sasa akiwa ndani ya Kanisa Lake, Bibi-arusi Wake. Mnaona, wanaungana pamoja. Ni wakati

wa kuungana. Makanisa yanaungana, mataifa yanaungana, na Bibi—arusi na Kristo wanaungana. Mnaona, ni wakati wa kuungana.

²⁷⁵ Sasa aminini tu, kirahisi. Usijaribu kuwa na wasiwasi na kukazana kwa kitu fulani, maana hupati chochote. Se—sema tu kwa unyenyekevu, “Bwana, ninaamini.” Mtu fulani na afanye hivyo tu. Na sasa mimi . . .

²⁷⁶ Ni wangapi wameketi mbele yangu, hasa . . . Sasa, ninawajua watu hawa *hapa*, na hawa *hapa*. Ninajua wengine wanaoketi *hapa*. Vipi kuhusu papa *hapa*, papa hapa tu mbele zangu? Hebu na tulishughulikie kundi hili dogo papa *hapa* mahali fulani. Ni wangapi hawajapata kumwona Kristo akijitambulisha namna hiyo, kwa . . . Hebu na tuone mikono yenu, “Hamjapata kuona hilo.” Nadhani kila mtu ameona. Vema.

²⁷⁷ Ninyi ombeni sasa. Sasa iweni tu na kicho. Sijui kwamba Yeye atafanya hivyo. Siwezi kusema hivyo. Ni juu Yake. Je! itawafanya mwamini, sana? Bwana anasikia hayo. Anajua mambo yote.

²⁷⁸ Mtu huyo anayeketi papo hapo, anayeumwa na ngiri. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya hiyo ngiri? Unaamini? Sisi hatufahamiani, nafikiri, mimi na wewe. Sikujui. Sijawahi kukuona. Lakini kama hilo ndilo ulilokuwa ukiomba, inua mkono wako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mtu huyu anayeketi . . .

²⁷⁹ Je! unaamini ya kwamba—unaamini ya kwamba wakati Andrea alipokuwa amemwambia Simoni aje aone ya kwamba walikuwa wamemwona Masihi, na wakati alipokuja Mbele za Bwana Yesu? Kwa kuwa unawasiliana na kitu Fulani sasa, maombi yako. Unaona, Yeye alimwambia kwamba yeye alikuwa ni nani. Je! unaamini Mungu angeweza kuniambia kwamba wewe u nani? Kama utaamini jambo hilo, Yeye anaweza kufaya hivyo. Je! hilo lingekutia moyo kuamini kwa moyo wako wote? Ninyi wengine lingewafanyia vivyo hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁸⁰ Sasa mtu huyu ameinua mkono wake juu, ya kwamba yoyote aliyoambiwa . . . Sijui; itanibidi kucheza kanda hii, mnaona. Chochote kile kilichokuwa, kilikuwa ni kweli. Hilo ni kweli, bwana? [Huyo ndugu anasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Chochote kile kilichokuwa, ni kweli.

Bw. Shepherd, amini kwa moyo wako wote. “Kama unaweza kuamini.”

²⁸¹ Sasa hivyo si zaidi ya alivyosema, “Jina lako ni Simoni, mwana wa Yona.” Sasa kama tu utaamini, hilo tu ndilo linalotakiwa. Unaona? Sasa ni kitu gani? Yeye aliahidi jambo hilo. Alitoa hiyo ahadi. Hiyo inaonyesha ya kwamba Yeye yupo hapa. Si mimi tu; Yeye yumo ndani yenu. Yeye yumo ndani ya Mwili Wake wa waaminio.

282 Maskini mama, unayelia na kuomba, ukiwa umeinamisha kichwa chako. Unaugua kansa. Kama hutaogopa, na utaamini, Mungu atakuponya kama unaweza kuamini jambo hilo. Ataukosa, hakika. Bibi Hood, amini kwa moyo wako wote sasa, ya kwamba Yesu Kristo anakuponya, nawe unaweza kupata uliyoomba. Sasa utaamini kwa moyo wako wote? Amina.

283 Yupo mama anayeketi papo hapo karibu na wewe pale anayeumwa na tumbo, ugonjwa wa moyo, matatizo mengi. Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupokea uponyaji wako. Je! unaamini kwa moyo wako wote, utaukubali? Unaukubali? Vema.

284 Mwanamume huyo pale mwenye kikundu, je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya bawasiri hizo na kukufanya mzima? Simama.

285 Unafikiri nini juu ya jambo hilo, unayeketi karibu naye hapo, ukiwa na ngiri? Je! unaamini Mungu anaweza kuponya hiyo ngiri na kukufanya mzima?

286 Mama aliye papo hapo karibu na mkono wako, anaumwa na kichwa. Yamekwisha sasa. Sivyo? Unaona, imani yako ilifanya jambo hilo. Hivyo ndivyo tu inavyokupasa kufanya, ni kuamini tu.

287 Huyu hapa mama mwenye kisukari. Je! unaamini Mungu atakuponya, mama, unayeketi hapo ukiwa na kisukari? Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Unaamini? Bibi Robinson. Hilo ndilo jina lako.

288 Weka mkono wako juu yake pale kwa ajili ya hiyo ngiri, labda Mungu atamponya, pia. Kama unaamini! Utaamini? Vema, bwana.

289 Bibi anayeketi karibu na wewe, weka mkono wako juu yake, bwana, ana uvimbe wa neva. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya uvimbe huo wa neva na kukuponya? Unaamini, unaweza kupokea uponyaji wako, pia. Huna budi kuamini.

290 Sasa hilo ni thibitisho. Mungu alitoa ahadi, sasa ni wangapi wanaoamini ya kwamba Kristo yupo hapa? Mnaamini jambo hilo? Sasa, ninyi nyote mnaotaka, mlio Mbele Zake sasa, mnaotaka rehema kutoka Kwake, mnaotaka rehema nafsi mwenu, na mnataka kumkubali sasa wakati mkiwa moja kwa moja Mbele Zake, ametambulishwa. Sasa mimi. . .

291 Huenda mtu akaingia hapa akiwa na makovu ya misumari mikononi mwake, na alama za miiba na kusema, "Mimi ndiye Bwana." Maskini mnafiki yeyote anaweza kufanya jambo hilo. Lakini, ule Uzima! Mwili wa Bwana Yesu umeketi mkono wa kulia wa Ukuu; wakati atakapokuja, hakuna wakati tena, wakati mwili huo utakaporudi duniani. Lakini Roho Wake yupo hapa, Uhai Wake unatoa thibitisho Lake kwamba Yeye yupo

hapa. Mnaona? “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

²⁹² Nanyi mnaotaka rehema kutoka Kwake sasa, je! mwaweza kusimama tu kwa ajili ya maombi? Kote jengoni, ninyi ambao . . . popote ulipo, ungeweza kusimama? Mungu awabariki, huko nyuma kule ndani. Hiyo ni kweli, endeleeni tu kusimama. Simameni tu kwa miguu yenu, hivyo tu ndivyo ninavyotaka mfanye. Simameni tu kidogo, kwa ajili ya maombi. Kama mngalisimama kwa ajili Yake! Kama mnamwonea aibu sasa, Yeye atawaonea aibu mbele za Baba; na kama mko—mko tayari kumkiri sasa, Yeye atawakiri mbele za Baba. “Sasa ninataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu. Ninamtaka anijaze kwa Roho Wake sasa hivi. Ninamtaka.” Endeleeni tu kusimama kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi, mkipenda. Simameni. Naam. Ninataka . . . Ninajisikia kuongozwa kufanya jambo hili, kufanya wi-. . .Huu ni wito wa madhabahuni. Simameni. Hatuna madhabahu ya kuendea, moyo wako ndio madhabahu. Ondoleeni mbali tu kutokuamini kote, na mjue ya kwamba Yeye yupo hapa sasa. Simameni kwa miguu yenu, ninyi mnaotaka kumkubali Kristo sasa hivi, katika Uwepo wa Kiungu unaouhisi, ambao umethibitishwa sasa.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁹³ Bwana Yesu, hao ni Wako. Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu.” Na sasa kulingana na sayansi, wasingeweza hata kuinua mkono wao; kanuni ya uvutano inasema mikono yetu haina budi kuning’inia chini. Lakini kuna uhai ndani yao, na uhai huo uliletwa karibu na Uzima wa Milele, Kristo. Nao walifanya uamuzi moyoni mwao, ya kwamba wamemalizana na ulimwengu. Nao wanainua mikono yao, na kusimama kwa miguu yao, wakiasi kanuni ya uvutano, ya kwamba mna uhai mle. Vivyo hivyo sisi nasi tunaasi kanuni ya ulimwengu na kutokuamini!

²⁹⁴ Katika Jina la Yesu Kristo, hao ni Wako. Hao ni tunu za upendo wa Injili. Hao ni kumbukumbu za Ujumbe huu, usiku wa leo, na ninii . . . Uwepo Wako mkuu pamoja na sisi. Yaweke majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, Huko, Bwana. Tunaomba kwamba—kwamba kila mmoja wao atakuwa Huko, kama watoto Wako, wapendwa Wako.

²⁹⁵ Wajaze kwa Roho Mtakatifu wa Mungu, ndani ya mioyo yao. Jalia maisha yao yajazwe sana na Nguvu za Mwenyezi Mungu, ili kwamba unyenyekevu na upendo na wema na utu wema vitiririke kutoka kwao, na bidii ya kuona wengine wakiokoka, ambao wakati mmoja walikuwa katika hali yao. Tujalie, Bwana.

²⁹⁶ Jambo pekee tunaloweza kufanya, Bwana, ni kuamini. Nao walisimama kama kumbukumbu la imani yao. Na sasa pamoja na imani yangu na imani yao, kwa pamoja, tunaiweka juu ya madhabahu Yako, kwa imani. Nao ni dhabihu iliyowekwa pale,

ikingojea Mwana wa Mungu aliyetolewa dhabihu kuwakubali waingie katika Ufalme Wake. Tujalie, Bwana. Hivi sasa tu jalia wawe Wako, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁹⁷ Sasa ninyi mnaomwamini kwa moyo wenu wote, mnaosimama, inueni mkono wenu, msemi, “Ninamwamini. Ninamkubali sasa hivi kama Mkombozi wangu, na ninatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Inua mkono wako. Mungu akubariki.

Sasa mnaweza kuketi.

²⁹⁸ Na ninawatakeni mwende zenu kwenye kanisa fulani, sasa, mara moja.

²⁹⁹ Kesho usiku tutafanya m—mkutano wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kesho usiku, papa hapa jengoni. Sasa, kuna ushabiki mwingi sana wanaouita ubatizo wa Roho Mtakatifu, bali hilo halimaanishi kwamba hakuna Roho Mtakatifu halisi. Kuna Roho Mtakatifu halisi na wa kweli wa Mungu, vivyo hivyo. Nami ninaamini ya kwamba atakutana na sisi hapa kesho usiku.

³⁰⁰ Sasa, ni wangapi humu jengoni wameshawishika tuko katika wakati wa mwisho? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wameshawishika ya kwamba hii ni Kweli, Neno linapaswa kuwa hivi katika siku za mwisho? Inua mkono wako. [“Amina.”] Ni wangapi wenu walio waaminio? Pungeni mikono yenu. [“Amina.”] Vema. Yesu alisema Maneno haya, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kama wewe ni mwaminio.”

³⁰¹ Sasa ni wangapi wanaomhitaji Kristo mwilini mwenu? Inueni mikono yenu. Vema, ninyi waaminio mnaoketi karibu nao, wekeaneni mikono nyinyi kwa ninyi. Na jinsi unavyoomba kanisani mwako, hivyo ndivyo utakavyoomba hapa. Usijiombee mwenyewe. Waombee; wao wanawaombea. Na Biblia ilisema, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Sasa ombeni jinsi mnavyoomba, na kwa ahadi.

³⁰² Bwana Yesu, hao ni wako. Wapokee katika Ufalme Wako. Na umponye kila mmoja, Bwana; na lesu hizi. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tujalie, Bwana. Shetani amepoteza ngome yake. Nguvu za Mwenyezi Mungu na zimponye kila mmoja. 

YEHOVA-YIRE ² SWA64-0403

(Jehovah-Jireh ²)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 3 Aprili, 1964, kwenye Kibanda cha Klabu ya 4-H huko Louisville, Mississippi, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org